KUCHUNGUZA SIFA ZA KIFANI ZA UTENDI WA KISWAHILI: MFANO UTENDI WA FUMO LIYONGO

ALI MUSSA FAKI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMLI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: ***Kuchunguza Sifa za Kifani za Utendi wa Kiswahili: Mfano Utendi wa Fumo Liyongo,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Digrii ya Uzamili MA (Kiswahili- Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

_____

Prof. Dkt. Sheikh T. S. Y. M. Sengo

(Msimamizi)

_____

Tarehe

HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba. .

TAMKO

Mimi, **Ali Mussa Faki** nathibitisha kwamba, hii ni kazi niliyoifanya mimi mwenyewe na kwamba haijawasilishwa katika chuo kikuu chochote kingine kabla kwa minajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

_____

Saini

_____

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapenzi, Mussa Faki Ali na Halima Ali Faki wa Kiungoni, Wete Pemba.

SHUKURANI

Kwanza kabisa, kabla sijasema lolote, ninapenda nitoe shukurani zangu zisizo na ukomo kwa ALLAH SUBHANAHU WATAALAH, kwa kunijaalia afya njema, katika kipindi chote cha juhudi yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika muda wote wa masomo yangu ya Uzamili. Ninasema, kwa unyenyekevu, Alhamdulillah Rabbillaalamina.

Pili, ninapenda kumshukuru kwa dhati, Msimamizi wangu, Prof. Sengo kwa kunilea kitaalimu na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno ila kumuombea duwa ya kheri.

Tatu, ninapenda kuwashukuru wafuatao; Prof. E. Mbogo, Dkt. Maulid na Bw. Bakar Kombo Bakar kwa msaada wao wa ushauri kimasomo. Nne, ninawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha na kunifunza maisha ya Dunia na Akhera. Vile vile, shukurani nyingi ni za mke wangu kipenzi, Bi Maua Hemed Hamad na watoto wangu; Mussa Ali Mussa, Ahmed Ali Mussa, Halima Ali Mussa, Hafsa Ali Mussa na Maryamu Ali Mussa, kwa uvumilivu wao, huruma na kunitia moyo katika kuendeleza masomo yangu.

Mwisho, ninawashukuru ndugu zangu na wanachuo wenzangu wote, wote walioshiriki moja kwa moja na kwa namna yoyote, kunisaidia katika kuikamilisha kazi hii.

IKSIRI

Utafiti huu unahusu kuchunguza sifa za kifani za Utendi au Utenzi wa Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza vipengele vya fani kama vile; muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha katika Utendi wa Kiswahili. Mfano, *Utendi wa Fumo Liyongo*, ili, kuona ni jinsi gani sifa za kifani zinavyojidhihirisha katika tenzi za Kiswahili. Utafiti huu ulitumia mbinu ya Maktaba. Wateuliwa wa utafiti huu walipatikana kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalumu. Aidha, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Utafiti huu umegundua kuwa tenzi za Kiswahili, zina sifa za kifani mahususi. Utafiti huu umegundua kuwa, neno na dhana *tenzi* ni sawa na *tendi* miongoni mwa jamii za Waswahili. Aidha, utafiti umegundua kuwa, tenzi za Kiswahili, zina sifa za kifani zinazofanana. Kwa mfano, zote zina mianzo na miishio inayofanana, ya kuanza kwa duwa na kumaliziya kwa duwa. Huwa na muundo na mtindo wa baharu ya Utendi. Utenzi, huweza kuwapo au kutakuwapo mhusika shujaa. Aidha, utafiti umegundua kuwa, tenzi za Kiswahili, hazia urefu mahususi au idadi maalumu ya beti. Sifa nyengine ni uunganifu na mapisi ya kweli. Pia, huwa una maudhui makubwa ya Dini ya Kiislamu. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuundo na Nadharia ya Ujumi wa Kiafrika katika kufikisha lengo lake.

YALIYOM0

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKI MILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKSIRI ..... **vii**

YALIYOM0 ..... **viii**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI WA JUMLA **1**

1.0 Utangulizi **1**

1.1 Mada ya Utafiti **3**

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti **3**

1.3 Tatizo la Utafiti **5**

1.4 Lengo la Utafiti **5**

1.4.1 Madhumuni Mahususi **6**

1.5 Maswali ya Utafiti **6**

1.6 Umuhimu wa Utafiti **6**

1.7 Mipaka ya Utafiti **6**

1.8 Vikwazo vya Utafiti **7**

1.9 Utatuzi wa Vikwazo **7**

SURA YA PILI **8**

UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA **8**

2.0 Utangulizi 8

2.1 Dhana ya Utendi. 8

2.1.1 Vielezea vya Utendi/Utenzi wa Kiswahili. 10

2.1.2 Mapisi katika Tendi za Waswahili 11
2.1.3 Maudhui ya Dini 12
2.1.4 Milango ya Kulisomesha Somo la Fasihi. 12
2.2 Dhana ya Fani 14
2.3.1 Muundo 15
2.3.1.1 Muwala 15
2.3.1.2 Kipande 15
2.3.1.3 Mshororo 16
2.3.1.4 Kibwagizo 16
2.3.1.5 Bahari ya Utendi 16
2.3.1.6 Ubeti 17
2.3.1.7 Urari wa Mizani 17
2.3.1.8 Vina 17
2.3.2 Mtindo 18
2.3.2.1 Uteuzi wa Maneno 18
2.3.2.2 Mpangilio wa Maneno 19
2.3.2.3 Takiriri 19
2.3.2.4 Wizani 20
2.3.3 Matumizi ya Lugha katika Utendi 20
2.3.3.1 Taswira. 21
2.3.3.2 Maswala ya Balagha 21
2.3.3.3 Tabdila 21
2.3.3.4 Mazida 22
2.3.3.5 Iksiri 22
2.3.3.6 Kinaya 22
2.3.3.7 Sitiari 22

2.3.3.8 Tashibiha 23
2.3.4 Wahusika 23
2.3.5 Mandhari 23
2.3.6 Kuhusu upekee wa Utendi/ Utenzi 24
2.3.7 Mapisi ya Fumo Liyongo 25
2.4 Uchaguzi wa nadharia 25
2.4.1 Nadharia ya Umuundo 26
2.4.2 Nadhariaya Ujumi wa Kiafrika 26
SURA YA TATU 28
MBINU ZA UTAFITI 28
3.0 Mbinu za Utafiti 28
3.1 Eneo la Utafiti 28
3.2 Uteuzi wa Data 28
3.3 Wateuliwa 28
3.4 Mbinu za Kukusanya Data 29
3.4.1 Mbinu ya Maktabani 29
3.5 Vifaa vya Utafiti 29
SURA YA NNE 31
UCHAMBUZI WA DATA 31
4.0 Utangulizi 31
4.1 Uchambuzi wa Data 31
4.1.1 Bahari ya Utendi 32
4.1.2 Mianzo na Miisho ya Kifomula 32
4.1.3 Uunganifu 33
4.1.4 Wingi wa Beti 34
4.1.5 Kielezea cha Kuwapo au kutakuwapo kwa Shujaa 35

4.1.6 Mapisi katika Utendi wa Fumo Liyongo 36
4.1.6.1 Mapisi ya mhusika Fumo Liyongo 36
4.1.7 Dini katika Utendi wa Fumo Liyongo 38
4.2 Fani katika Utendi wa Fumo Liyongo 38
4.2.1 Mandhari 39
4.2.1.1 Mandhari katika Utendi wa Fumo Liyongo 39
4.2.1.2 Mandhari ya gerezani 39
4.2.1.3 Nyumbani kwa Mfalme 41
4.2.1.4 Mandhari ya Nyikani 41
4.2.1.5 Mandhari ya Mji wa Pate 42
4.3 Wahusika katika Utendi wa Fumo Liyongo 43
4.3.1 Fumo Liyongo 43
4.3.2 Sultwani 46
4.3.3 Mama yake Liyongo 46
4.3.4 Mtoto wa Kambo wa Liyongo 47
4.3.5 Sada 48
4.3.6 Askari 48
4.3.7 Wagala 49
4.4 Matumizi ya lugha katika *Utendi wa Fumo Liyongo* 49
4.4.1 Tashibiha 50
4.4.2 Mubalagha 51
4.4.3 Sitiari 52
4.4.4 Kinaya 52
4.4.5 Taswira 54
4.4.6 Balagha katika *Utendi wa Fumo Liyongo* 54
4.4.7 Tabdila 55

4.4.8 Mazida....56
4.4.9 Iksiri....56
4.5 Muundo katika Utendi wa Fumo Liyongo....57
4.5.1 Mishororo....57
4.5.2 Bahari ndogo....57
4.5.4 Mizani....58
4.5.5 Vina....59
4.6 Mtindo katika Utendi wa Fumo Liyongo....59
4.6.1 Mianzo ya kifomula....60
4.6.2 Kiswahili cha Asili....60
4.6.3 Takiriri....62
4.6.3.1 Takiriri Neno....62
4.6.3.2 Takiriri Kina....64
4.7 Upekee wa Utendi wa Fumo Liyongo....67
4.7.1 Shujaa wa Mapisi ya Waswahili....67
4.7.2 Mgogoro wa Utawala katika Eneo la Waswahili....67
4.7.3 Usaliti wa Mtoto kwa Baba yake wa Kambo....68
4.7.4 Matumizi ya Mhusika mwenye Nguvu na Uwezo wa Kimaajabu....68
SURA YA TANO....69
MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO....69
5.0 Utangulizi....69
5.1 Muhtasari....69
5.1.1 Madhumuni Mahsusi ya Kwanza....69
5.1.2 Madhumuni Mahsusi ya Pili....71
5.1.3 Madhumuni Mahususi ya Tatu....73
5.2 Hitimishi....74

5.3 Mapendekezo ya Utafiti 74

5.3.1 Kwa Watunga Mitalaa 74

5.3.2 Walimu 75

5.3.3 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 75

MAREJELEO 76

NYONGEZA 79

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusu kuchunguza sifa za kifani za Utendi/Utenzi wa Kiswahili mfano; Utendi wa Fumo Liyongo. Utafiti una sura tano. Sura ya kwanza, inaelezea mambo ya msingi kuhusu mada, Usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na namna vikwazo hivyo vilivyotatuliwa. Aidha, sehemu ya pili imeelezea kazi zilizosomwa na mtafiti, zinazohusina na mada iliyotafitiwa. Pia, sehemu hiyo, imeelezea Nadharia zilizomuongoza mtafiti katika utafiti huu. Sehemu ya tatu imeelezea mbinu zilizotumika kukusanya data na kuzichambua. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu ya Maktabani, uteuzi lengwa, kazi iliyoteuliwa; ambayo ni Utendi wa Fumo Liyongo.

Aidha, imeelezwa kwamba, data za utafiti huu, zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Sura ya nne imeshughulikia uchambuzi wa data zilizokusanywa na mtafiti. Sura ya tano inaelezea matokeo ya utafiti. Sehemu hiyo, mtafiti alitathmini madhumuni ya utafiti. Pia, kumeelezwa mapendekezo ya utafiti.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Utenzi au Utendi ndiyo utanzu mmoja wapo wenye historia ndefu katika Ushairi wa fasihi ya Kiswahili. Upana wa historia yake, umefanya ugumu wa kuuzungumzia. Utenzi ni utanzu ambao umechunguzwa na watafiti wa ndani na wa nje ya bara hili la Afrika, kama vile; Finnegan (1970), Mulokozi (1999), King`ei (2001), Foibe (2013), Chaligha (2013) na Ndumbaro (2013). Mapisi ya Utenzi/Utendi wa Kiswahili yamekuwa ni kitandawili kikubwa. Kwa mfano, baadhi ya tungo, ambazo zilitungwa kabla ya kuja wageni katika bara la Afrika, tenzi hizo zilikuwa zikikaririwa kwa vinywa tu kabla ya hatma ya kuandikwa. Mulokozi (1999), anaeleza kuwa, Utendi

wa Fumo Liyongo, ni Utendi uliyotungwa na Mohamed Kijumwa katika mwaka 1913. Kumekuwako sababu nyingi za kutushawishi tukiri kuwa, kisa hicho kilikuwa kikisimuliwa kabla ya kutiwa maandishini katika bahari ya Utenzi. Inasadikiwa, katika kulifanya hilo, kisa hicho kilisahaulika pakubwa na kubakia tu, katika visehemu vidogo vidogo vya kughaniwa si cha kuandikwa. Kwa hiyo, Mohamed Kijumwa ni mkusanyaji na mhariri zaidi kuliko kuwa yeye ndiye mtunzi.

Kwa mujibu wa wahakiki kama vile, Mulokozi (1999), anaelzea kuwa, Utendi wa kwanza ni Hamziya. Pia, kwa upande mwengine, wapo wanaosema kuwa, utungo wa mwanzo wa Utendi/Utenzi ni Utendi wa Mwana Munga. Huo ndio Utendi wa zamani sana, na ulitungwa mwaka 1517. Hata hivyo, tarehe hizo zinahitaji kufanyiwa utafiti zaidi, kwa kuwa, mpaka leo, watafiti wamekuwa wakitafautiana kuhusu tarehe hasa, aliyoishi Liyongo. Hivyo, watafiti kama vile, King`ei (2001), Mulokozi (1999), wanaona kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo* ni msingi mkuu wa kuchunguza historia ya Utenzi wa Kiswahili.

Wamitila (2002), anaeleza kuwa, tenzi nyingi za Kiswahili zinafanana kidhamira na kifani. Asilimia kubwa ya tendi za Kiswahili, zina maudhui ya dini ya Kiislamu. Kimtindo zinafanana kwa kutumia fomula ya fasihi, fomula sawa za ufunguzi na ufungizi, kwa mfano, tendi zote za Kiswahili huanza kwa duwa na kumaliza kwa duwa, msuko na mgogoro wa msuko unaokaribiana. Pia, kuna matumizi ya lugha ya Kiswahili asilia, cha Amu na cha Pate. Ingawa, tenzi za wakati huo, zilitegemea lugha ya mtunzi, tenzi za Kiswahili, zina matumizi mapana ya msamiati wa lugha ngeni, hasa Kiarabu cha Allah (S.W) kilichowafikiya Waswahili kupitiya mlango wa Qur ani Tukufu. Pia, Kiarabu hicho kiliwafikia Waswahili kutokana na shughuli kama vile Biashara, Safari, Visomo, Ndoa na Maisha. Na unyambuaji wa maneno wa kiwango cha juu.

Vile vile, Utenzi hutungwa kwa kuzingatia mpangilio maalumu wa beti, idadi maalumu ya mizani, katika kila mshororo, ukamilifu na upatanifu wa vina na mizani. Hakika, Utendi/ Utenzi wa Waswahili, unasemekana kuwa, una ujumi wa kipekee katika ulimwengu wa fasihi. Kwa sababu, Arudh hiyo ya Kiswahili, ina urari wa vina na mizani, ambayo huufanya uimbike kwa sauti moja, tangu mwanzo wa Utendi hadi mwisho wa Utendi.

Pamoja na kwamba, Utenzi wa Kiswahili ni utanzu wa kale sana na maarufu sana, hakujaonekana marejeleo ya kitaalimu, kuhusu sifa za kifani, za Utendi wa Kiswahili. Hivyo, katika utafiti huu, sifa za Utendi/Utenzi wa Kiswahili zilichunguzwa, ili kupunguza tatizo la uhaba wa marejeleo yanayohusiana na mada hii.

1.1 Mada ya Utafiti

Kuchunguza sifa za kifani za *Utendi wa Kiswahili : Mfanno Utendaji wa Fumo Liyongo*

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996 na 1999, na King`ei 2001), *Utendi wa Fumo Liyongo* ulitungwa na Bwana Muhamad bin Abubakar bin Omar, anayejuilikana zaidi kwa jina Mohamad Kijumwa, mwaka 1913. *Utendi wa Fumo Liyongo*, unahusu mgogoro kati ya Liyongo na kaka yake, Mfalme wa Pate, ambaye katika baadhi ya maandishi, anatajwa kwa jina la, Daudi Mringwari. Mgogoro huo, ulizuka, baada ya Fumo Liyongo kuwa maarufu, miongoni mwa Wagala. Hivyo, Mfalme Mringwari, alikhofu kunyang`anywa utawala wake.

Kutokana na hali hiyo, Mfalme alitumia kila mbinu, ili kuhakikisha amemdhibiti Fumo Liyongo. Juhudi nyingi alizozitumia Mfalme, hazikufanikiwa kuondoa maisha ya Fumo Liyongo. Mwisho, Mfalme aliamua kumtumia mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo ili kumuua baba yake. Baada ya kuahidiwa uongozi, mali na kuozeshwa binti wa Mfalme, mtoto alimfuata baba yake na kuidodosa siri ya kile ambacho kingeweza kumuua. Baada ya kupata siri hiyo, Mfalme akampa mtoto huyo, sindano ya shaba ili kumchoma baba yake kitovuni. Mtoto alifanikiwa kumchoma baba yake sindano hiyo na kumuua. Mfalme alipopata taarifa za kifo cha Fumo Liyongo, aliamua kumfukuza mtoto huyo. Mwisho, mtoto wa Fumo Liyongo akapata maradhi, naye akafariki.

Utenzi, pia hujuilikana kwa jina la Utendi, umewahi kufanyiwa utafiti na wataalamu wa ndani na wa nje ya bara la Afrika. Mmoja kati ya watafiti waliowahi kufanya utafiti juu ya tenzi/tendi za Kiswahili ni Mulokozi (1999). Katika utafiti wake, Mulokozi aliona dhana ya Epiki ya Kiengereza kuwa sawa na dhana ya Utendi wa Kiswahili, dhana ambazo ni tafauti kabisa. Dhana ya Epiki, yenye maana ya hadithi refu, si sawa na dhana ya Utendi. Ukweli ni kwamba dhana ya Utendi na dhana ya Utenzi, tafauti ni matamshi tu, Kaskazini; yaani eneo la Upwa wa Afrika Mashariki kama vile katika mwambao wa Kenya, hutumika zaidi “Utendi” na Kusini; eneo la Uswahilini Tanzania hutumika zaidi “Utenzi,” Hivyo, katika utafiti huu mtafiti alizitumia dhana hizo kuwa ni sawa sawa.

Sababu zilizomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu, ni kutokana na watafiti waliowahi kufanya utafiti kuhusu tendi za Kiswahili, baadhi yao wakichanganya dhana ya Epiki na tendi za Waswahili kuwa ni dhana moja, kama alivyofanya Mulokozi (1999), jambo ambalo si sahihi. Hadi sasa, baada ya mtafiti kufanya utalii wa kina, ameona kuwa, hakuna utafiti wa kina uliyofanyika kwa lengo la kuchunguza sifa za Utendi za Utendi

wa *Utendi wa Fumo Liyongo*, jambo linalodhihirisha uhaba wa machapishi yanayohusiana na sifa za Utendi huo. Hii ni kusema kuwa, sifa za kifani za *Utendi wa Fumo Liyongo* . Kutokana na hivyo, mtafiti amechunguza sifa za kifani za Utendi *Utendi wa Fumo Liyongo,* ili kuziba pengo hilo la kitaalimu.

1.3 Tatizo la Utafiti

Utendi/Utenzi ni utanzu maarufu sana katika jamii za Waswahili. Utenzi huimbwa katika sherehe kama vile harusi, sherehe za kuwapokea viongozi wa serikali, katika mikutano ya kisiasa na hata katika mikutano ya wanajamii. Pamoja na umaarufu huo wa tendi za Kiswahili, katika utalii uliyofanywa na mtafiti, hakujaonekana utafiti wa kina uliowahi kufanyika kwa lengo la kuchunguza sifa za kifani za Utendi wa Kiswahili, mfano wa *Utendi wa Fumo Liyongo*.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), Finnegan (1970) alichunguza fasihi ya Afrika na kufikia kauli kuwa Afrika haikuwa na epiki. Kuanzia hapo, wataalamu kama vile Okpewho (1976), na Mulokozi (1999), walifanya utafiti na kuchunguza epiki na kuchanganya dhana ya utendi kuwa sawa na dhana ya epiki ya Waengereza. Kwa mfano, Mulokozi (1999), alifanya utafiti juu ya tendi/tenzi za Kiswahili, akadai kuwa Afrika inazo epiki kwa maana ya tendi, dhana ambazo ni tafauti kabisa. Hivyo, tunaona kuwa sifa za kifani za Utendi wa Kiswahili bado hazijuilikani kwa kina. Utafiti huu, hivyo basi, umefanywa ili kuziba pengo hilo.

1.4 Lengo la Utafiti

Kuchunguza, kuchambua na kuzidhihirisha sifa za Utendi wa Kiswahili kwa kutumia vipengele vya fani katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

1.4.1 Madhumuni Mahususi

i) Kuchunguza sifa zinazopatikana katika Utendi wa Fumo Liyongo

ii) Kufafanua vipengele vya fani, vinavyojitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

iii) Kuelezea sifa za kipekee za *Utendi wa Fumo Liyongo.*

1.5 Maswali ya Utafiti

i) Utendi wa Fumo Liyongo una sifa zipi?

ii) Je, ni vipengele vipi vya fani vimetumika katika *Utendi wa Fumo Liyongo?*

iii) *Utendi wa Fumo Liyongo* unasifa zipi za kipekee?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu ufuatao:

Umuhimu wa utafiti kitaalimu: Utafiti huu unatarajiwa uwasaidie kupata maarifa mapya yanayohusu tendi za Kiswahili wahadhiri, walimu, wanafunzi pamoja na watafiti kwa taarifa muhimu kuhusu sifa za fani zinazohusiana na tanzu za Arudhi ya Kiswahili.

Umuhimu wa utafiti kinadharia: Utafiti huu unathibitisha sifa za kifani za Utendi wa Kiswahili kwa kutumia *Utendi wa Fumo Liyongo.*

1.7 Mipaka ya Utafiti

Katika utafiti huu, kulichunguzwa, sifa za kifani za *Utendi wa Fumo Liyongo.* Vipengele vya fani vilivyofanyiwa uchunguzi, ni pamoja na wahusika, muundo, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha. Uchunguzi huu uliongozwa na Nadhariaya Umuundo na Nadhariaya Ujumi wa Kiafrika. Ilichaguliwa Nadhariaya Umuundo, ili kumuongoza msanii kubaini namna fani ya Utendi wa Kiswahili inavyoundika na kukamilishana.

Aidha, Nadhariaya Ujumi wa Kiafrika ilimuongoza mtafiti, ilikuona namna fani katika tenzi za Kiswahili inavyoibua ujumi wa Waswahili katika tenzi.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Ugumu wa kupatikana kwa marejeleo kama vile tasnifu zilizokwisha kuandikwa kuhusu mada hii. Hii ilitokana na kutokuwako, hapa Kisiwani Pemba, Maktaba zenye kuhifadhi tasnifu za kazi tangulizi. Uchanga wa usomi wa daraja za Uzamili na Uzamivu, ndiyo kwanza umeanza. Maandalizi hayajafanywa na SUZA- Chuo Kikuu cha Serikali kilichokuwako, ambacho hakijaweza, hadi sasa, kuishawishi Wizara ya Elimu, kuimarisha vyanzo vyake vya utafiti.

1.9 Utatuzi wa Vikwazo

Kikwazo hiki kilichomkabili mtafiti, kiliweza kutatuliwa kwa kutumia mtandao wa wavupepe, pale ulipopatikana, ambao uliweza kusaidia kupata marejeleo yaliyohusu mada hii inayofanyiwa utafiti. Aidha, Maktaba ya serikali na za shule zilisaidia katika kutatua tatizo hili la marejeleo. Msimamizi binafsi, alitoa msaada wa kulipunguza tatizo hili kwa vile, jungu kuu halikosi ukoko.

1.10 Hitimisho

Sura hii ilieleza mambo ya msingi ya Kiutangulizi. Sura imeelezea utangulizi wa jumla, mada ya utafiti, usuli wa mada ya ufatifi, tatizo la utafiti, lengo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti.

SURA YA PILI

UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Utalii wa kazi tangulizi kwa Kiswahili sahihi cha asili, ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Utalii wa kazi tangulizi lazima uoneshe uhusiano wa maandishi hayo na mada inayofanyiwa utafiti. Ndani ya utalii wa kazi tangulizi , hupatikana Nadharia za utafiti, Nadharia ya njia za utafiti, Nadharia ya uchambuzi wa data. Aidha, utalii huo wa kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana, kwa kuzamia mbizi maandishi hayo ya huko nyuma na kufananishwa na taarifa hai zipatikanazo katika utafiti wa sasa wa data za awali zitokanazo na usaili wa ana kwa ana, ama data za majibu ya mahojaji (Sengo, 1985).

Baada ya kuelezea kazi ambazo zimeandikwa, zinazohusiana na mada ya utafiti huu, mtafiti alielezea Nadharia ya Muundo na Nadharia ya Ujumi wa Kiafrika ambazo zilimuongoza katika utafiti huu.

2.1 Dhana ya Utendi.

Chaligha (2013), anaeleza kuwa, kumetumika fomula, kuelezea maana ya Utendi kuwa ni E = M + Ms yaani (Epic= Mars + Music/muse), yaani Utendi ni mungu, Muziki na Vita (U=M+V). Akifafanuwa maelezo hayo, Chaligha (kashatajwa), anasema Utendi ni tukio la kimuziki linalozungumzia vita na miungu.

Mawazo hayo yana mashaka, kwa upande wa Utendi/Utenzi wa Kiswahili. Uswahilini, Utendi na Utenzi, tafauti ni matamshi. Tendi Uswahilini si lazima zizungumzie miungu

kama aonavyo Chaligha. Uswahilini kote, neno “miungu” ni kufuru. Kwa upande mwengine, fasili hiyo imedokeza suala muhimu la *kimuziki* na la *vita* ambalo linajidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

Chaligha (ameshatajwa), alieleza kuwa, tendi simulizi ni tungo simulizi zenye mtindo wa kifomula, zinazohusu mambo ya ajabu, ya watu wasio wa kawaida. Masimulizi hayo yanasimuliwa kwa njia ya mdomo. Utendi/Utenzi wa Kiswahili hughaniwa katika miktadha mingi kama vile, sherehe na msiba.

Mulokozi (1999), anaeleza kuwa, Utendi ni utungo mrefu wa kishairi wenye kusimulia hadithi ya ushujaa na mashujaa. Kwa jumla, Mulokozi anaona kuwa, Utendi lazima uwe na mhusika shujaa. Mawazo hayo, hayana ukweli wa moja kwa moja kuhusiana na Utendi wa Kiswahili.

Kwa hali hiyo, katika uchunguzi huu, sifa za usimulizi, sifa za kifomula, na hayo mambo ya ajabu yasiyo ya kawaida na urefu, yalichunguzwa, ili kuona namna kauli hizo zisivyojidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*.

Wamitila (2010), anaelezea kuwa, Utendi ni aina ya Utenzi ambao, unazungumzia maisha na matendo ya ushujaa au ya mashujaa wa jamii fulani. Tendi ni simulizi, ambazo husimuliwa na mtunzi na ambazo huchukuwa mkondo unaofanana katika kazi za kishairi. Mawazo ya Wamitila yametoa muelekeo tafauti na wa Mulokozi (ameshatajwa), juu ya dhana ya Utendi. Utendi/Utenzi na Nathari au Tutumbi hukutana kwenye maudhui lakini si kwenye fani, kila utanzu una mitindo, miundo, kanuni, ada na taratibu zake. Uswahilini, hakuna Utendi ama Utenzi wa kinathari au kitutumbi.

Utendi/Utenzi ni bahari kuu na kongwe ya Ushairi wa Kiswahili. Kusilazimishwe swala na mbuzi- mmoja na wapili ni wa majumbani.

Mawazo ya Wamitila (2010), yana upungufu. Kuna vielezea vya Utendi, havikuhusishwa katika ufafanuzi wake. Vielezea hivyo ni sifa za pekee za fani za Utendi wa Kiswahili, kama vile; muundo wa beti, bahari ndogo ya kila ubeti, vina na mizani pamoja na urefu wa Utendi huo. Hivyo, katika utafiti huu, vimechunguzwa vipengele vya muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha, ili kuona namna hayo yalivyojidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

Baada ya kutalii mawazo ya wanataalimu waliotangulia, dhana ya Utendi imeweza kuelezeka kwa kupambanuliwa kwa sifa ya Utendi/Utenzi ambao hufuata kaida ya urari wa vina na mizani na huweza kuwa na mhusika shujaa au asiyekuwa shujaa. Mhusika huyo mkuu, huitwa nguli. Vile vile, tendi, huelezea masuala yanayoihusu jamii, kama vile, masuala ya kijamii, ya kisiasa, ya kiuchumi na ya kiutamaduni. Masimulizi hayo, hutolewa kwa lugha ya kishairi, ambayo ujumi wa lugha hiyo, hutegemea jamii inayohusika na masimulizi yenyewe yanayotolewa huwa kwa ajili ya jamii, ili kuwa katika mwenendo bora wa maisha ya hapa Duniyni na Akhera.

2.1.1 Vielezea vya Utendi/Utenzi wa Kiswahili.

Fasili ya dhana ya fasihi imeibua mjadala miongoni mwa wanataalimu wa Kiswahili. Kuifasili fasihi kwa A= B, hakukubaliki, kwani, B si sawa na A, kwa hivyo, vielezea vya Utendi/Utenzi wa Kiswahili kama vilivyoelezwa na Sengo na Nabhany (2009), ni upwani, ujumi, ubunifu, usanii, vina, mizani, lugha ya mvuto, dhamira zenye athari, bahari, mikondo, mishororo, beti, utungo, ulinganifu, vipande, unyoofu, na mkato wa lugha, fikra nzito, telezi, tamu, tumbuizi, mawazo, hisiya, matukio, muwala, urari,

kanuni au misingi, nyimbo, Utenzi, mlingano wa sauti, ufupizi, kitulizi/ kikerezi moyo, hekima, mnato, umbo maalumu au bahari.

Maelezo hayo ya Sengo na Nabhany (2009), yanayotoa vielezea vya Utendi/Utenzi wa Kiswahili, yamesaidia sana kutoa mchango mkubwa katika kusukuma mbele uchunguzi wa sifa za fani za *Utendi wa Fumo Liyongo*. Ingawa vielezea hivyo vinahusu ushairi wa Kiswahli kwa jumla, Utenzi ukiwamo, lakini vielezea hivyo, vimemsaida sana mtafiti katika kuchunguza sifa za fani za *Utendi wa Fumo Liyongo*, kwa sababu, mtafiti alizichambua data alizozikusanya, ili kuona namna sifa hizo za vina, mizani, lugha ya mvuto, bahari ya Utendi, muwala, urari, mlingano wa sauti, ufupizi, umbo maalumu au bahari zinavyojidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

2.1.2 Mapisi katika Tendi za Waswahili

Kwa mujibu wa Edna (2013), kuwapo kwa historia katika tendi, kumewahi kuzua mitazamo tafauti miongoni mwa watafiti. Wapo wanaoona kuwa, hakuwezi kupatikana mapisi kwa maana ya historia ya kizungu, katika tendi, na kama itajitokeza mapisi, basi hayo si mapisi, kwa maana ya historia ya kizugu, bali ni masimulizi ya jadi tu ambayo hayana ukweli wowote. Mapisi ambayo ni kisasili, kama si kweli kamili ingepatikana wapi? Mawazo hayo yanamashaka. Sababu, i wazi. Fasihi ina ukweli uliyomo ndani ya jamii, ndiyo maana hutungwa kuiakisi.

Kwa upande mwengine, wapo wale wanaoona kuwa, tendi huweza kuelezea mapisi. Kwa mfano, Mulokozi (1999), anaeleza kuwa, tendi hutokana na historia, matukio ya kihistoria, na wahusika wa kihistoria. Kwa hivyo, mtafiti aliyatumia mawazo hayo, kukamilisha uchunguzi wake wa vipengele vya fani, kama vile wahusika, mandhari na matumizi ya luigha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, jinsi vinavyobainisha mapisi.

2.1.3 Maudhui ya Dini

Kwa mujibu wa TUKI (2004), dini ni imani inayohusiana na maumbo ya kiroho, kwamba kuna Muumba aliyeumba ulimwengu huu, na kwamba, ndiye Mtawala wa kila kilichomo. TUKI wanaongeza kwa kusema kuwa, ni mfumo fulani wa imani na njia ya kuabudu, kusali na kumtii huyo Muumba. Muhammad (2010), Uislamu ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kumpwekesha na kumfuata kwa kumtii na kujiepusha na Shirki na washirikina.

Ndumbaro (2013), alichunguza imani za dini katika *Utungo wa Mwindo*. Katika uchunguzi huo, alifikia hitimisho kuwa, suala la dini linajitokeza kwa kiasi kikubwa. Ndumbaro anaeleza kuwa, katika utungo huo, watu wanaabudu miunguu ya jadi. Ingawa kazi hiyo ya Ndumbaro ilihusu kazi nyengine tafauti kabisa na *Utendi wa Fumo Liyongo*, kazi hiyo iliweza kusukuma mbele utafiti huu, kwa kutuonesha namna ya kuchunguza masimulizi yanayohusiana na imani ya dini kwa kutumia vipengele vya fani.

2.1.4 Milango ya Kulisomesha Somo la Fasihi.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), anaeleza kuwa, dhana ya somo la fasihi imewahi kuibuwa mjadala mkubwa ulimwenguni; kuna wale wanaolisomesha somo hilo “ki-literature,” yaani “herufi” au “maandishi.” Kwa maana hayo, wale wanaoona kuwa, fasihi ni “literature,” wana mawazo kuwa, fasihi ni jumla ya maandishi yote yaliyomo bila kujali vielezea vya hiyo fasihi. Mlango huo unaingiza kila kilichoandikwa kuwa ni fasihi. Aidha mtazamo huo, huitenga fasihi ambayo haikuandikwa kuwa si fasihi. Vile vile, mawazo hayo yana maana kwamba, Afrika haikuwa na fasihi, na hivyo, fasihi ililetwa na wageni. Mawazo ambayo, hayakubaliki kabisa. Kwa sababu, Waafrika

walikuwa na Utamaduni wao na tanzu za Fasihi hata kabala ya kuja wageni. Wafrika hawakusubiri hadi walipokuja wazungu ndio wakaanza kujifunza fasihi.

Mlango wa pili wa kuifundisha fasihi, ni ule unaoeleza kuwa, fasihi ni taaluma ya sanaa ya maneno yenye vielezea vyake, ambayo ni pamoja na mazingira wanayoishi jamii ya watu, jadi za watu hao, ujumi, ubunifu, usanii, lugha na fasihi yao. Mlango huu, mbali na kutoa mwangaza juu ya fasihi, kwa kufafanua kuwa, fasihi ina vielezea vyake, pia imegusia maeneo muhimu ya dhana ya fasihi, iwe imeandikwa au haikuandikwa. Suala la njia za kuhifadhi, nalo ni pana, kwani kwa sasa, si maandishi au simulizi tu bali kuna na flashi, CD, kanda, wampepe na njia mpya za kimtandao. Kwa mtazamo huo wa Sengo (2015), kuna elimu moja tu ya fasihi ndani ya kila jamii ya Kiafrika. Aidha, maelezo haya yanatueleza kuwa, fasihi ni moja tu, hivyo, maandishi au masimulizi ni njia za uwasilishaji (Sengo, 2009). Kwa maelezo hayo, ni wazi, Waengereza walikuwa na dhana yao ya fasihi, kwa kuihusisha dhana hiyo na maandishi lakini literatue si sawa na “fasihi.”

Maelezo hayo yanayohusu milango ya kuifundisha fasihi, yalikua na umuhimu katika utafiti huu, kwa sababu, yanaweka wazi, upotoshaji wa kizungu kuhusu kuwapo kwa fasihi katika bara hili la Afrika. Waonavyo wao, ustaarabu ulianza na jamii zilizojuwa kusoma na kuandika. Kwa hivyo, Afrika, haikuwa na aina yoyote ya ustaarabu; ukiwamo huu wa fasihi. Hivyo, katika uchunguzi huu, mumeoneshwa sifa za kifani za *Utendi wa Fumo Liyongo* kama sehemu ya ujumi wa utamaduni wao uliyokuwapo, hata kabla ya kuingia kwa wageni katika upwa wa Afrika Mashariki. Kama Uengereza, wakaazi wa viamboni/Vijijini, waliitwa *Folk* na mila zao , *lore*, Afria kote Mijini na Vijijini, kulikaliwa na binaadamu na yao ni yao wote, wa hasi ni aliyekuwa mtomvu wa mema ya utamaduni wa jamii.

2.2 Dhana ya Fani

Wanataalimu na wahakiki wa fasihi kama vile, Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999), wanakubaliana kuwa, fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Mathalani, Wamitila (ameshatajwa), anasema kuwa, fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Fani hueleza mbinu na mtindo wakuyawasilisha maudhui yaliyomo.

Mulokozi (1996), anaona dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi, vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Maelezo hayo yana maana kuwa, fani ni mbinu, ambazo msanii huzitumia, ili, kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu. Maudhui na fani. Maudhui ni masuala yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Maudhui pia, hujulikana, kama yaliyomo. Kwa upande mwingine, fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Mbali na kuyawasilisha maudhui, fani pia, huwa na uamilifu wa kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi. Umbo lenyewe linaweza kuwa; la ndani au la nje.

Katika uchnguzi huu, mtafiti alishughulikia vipengele vya fani vinavyojidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Vipengele hivyo, hujenga umbo la nje. Umbo hilo ndilo linaloshughulikiwa zaidi katika tungo za Utendi/Utenzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), umbo la nje hujengwa kwa vipengele kama vile beti, mishororo, vina, mizani na kadhalika.

Utendi ni fani ya kisanii kama zilivyo fani nyengine za kifasihi kama vile; Hadithi Ndefu na Natiki. Utenzi hujengwa na mambo mawili makuu, fani na maudhui. Maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika tungo na fani ni njia anazozitumia mtunzi kuyawasilishia mawazo yake kwa hadhira yake (Mulokozi, 1996).

Mulokozi (1996), Mdungi (2000), Njogu na Chimerah (1999), wameelezea vipengele vya fani katika Utendi/Utenzi kama vifuatavyo:

2.3.1 Muundo

Njogu na Chimerah (1999), wanasema inapochunguzwa miundo ya Utendi/Utenzi, huangaliwa misitari, beti, mizani na vina. Urefu wa mshororo hutegemea idadi ya mizani. Ukubwa wa ubeti nao, hutegemea idadi ya misitari katika kila ubeti.

Muundo ni msuko, muingiliano na uwiano wa vipengele vyote vinavyojenga ushari au kazi nyengine ya sanaa. Vipengele vya nje vya muundo hudhihirika katika umbo la Utendi/Utenzi.

2.3.1.1 Muwala

Muwala ni upatanifu au uwiano mzuri katika mtiririko wa fikira za shairi au Utendi. Muwala ni mawazo ya shairi au Utenzi, yakifuatana kimantiki, ubeti hadi ubeti, na misitari kufuatana kwa mpangilio mzuri.

2.3.1.2 Kipande

Kipande ni sehemu ya mshororo (msitari) wa Utenzi (Utendi). Mshoro wa Utendi huwa umeundwa kwa kipande kimoja tu. Kwa mfano.

2.3.1.3 Mshororo

Mshoro ni msitari mzima wa Utendi wenye kujitosheleza, kimaana. Maana ya msitari, lazima iwe imekamililika katika kila msitari. Kamwe haipaswi kukatwa na kuendelezwa katika msitari mwengine. Kwa mfano:

226. Mui walisikitika
Hakuna wa kutosheka
Kwa Liyongo kutoweka
Imeanguka paziya.
(Kijumwa, 1913).

Mishororo hiyo hapo juu, kila mmoja umejitosheleza kimaana. Ingawa, wazo la msitari mmoja, linaweza kuendelezwa katika msitari mwengine.

2.3.1.4 Kibwagizo

Kibwagizo ni mshororo unaorudiwarudiwa mwishoni mwa ubeti, kwenye Utendi/ Utenzi. Mulokozi (1996), anaeleza kuwa, kazi ya kibwagizo katika Utendi, ni kumaliza ubeti na kushadidia dhamira au wazo kuu la shairi hilo.

2.3.1.5 Bahari ya Utendi

Bahari ndogo ya utenzi ni silabi inayojitokeza mwishoni mwa neno la mwisho la kila Ubeti hata zikiwa beti 10,000. Kwa mfano:

18. Mfalume kaandika
Waraka wake haraka
Mtu wake kampeka
Liyongo kampekeya.

50. Liyongo akatambuwa
Huzengea kukuuwa
Pale pate kayepuwa
Barani akitembeya.
(Kijumwa, 1913).

Katika beti zilizopo hapo juu, silabi “ya,” iliyoko mwishoni mwa msitari wa nne, ndiyo iitwayo *bahari ndogo* katika Utendi/ Utenzi.

2.3.1.6 Ubeti

Ubeti ni fungu la misitari lenye maana kamili. Ubeti waweza kulinganishwa na paragrafu katika maandish ya nathari. Utendi, kwa kawaida, huwa na misitari mine katika kila beti. Kwa mfano;

18. Mfalume kaandika
Waraka wake haraka
Mtu wake kampeka
Liyongo kampekeya.
(Kijumwa, 1913)

2.3.1.7 Urari wa Mizani

Urari wa mizani ni ulinganifu wa idadi ya silabi katika misitari. Kwa mfano, *Utendi wa Fumo Liyongo*, una mizani 8 iliyogawanyika, kipande kimoja kimoja.

Kwa mfano;

1 2 3 4 5 6 7 8
18. M/ fa/ lu me /ka/ a /ndi/ ka
Wa/ra/ka/ wa/ke /ha/ra/ka
M/tu /wa/ke /ka/m/pe/ka
Li/yo/ngo /ka/m/pe/ke/ya.
(Kijumwa, 1913)

Kazi kubwa za mizani ni, kwanza ni kuleta urari wa mapigo, pili, ni kuliwezesha shairi kuimbika, tatu, kuikamilisha dhana ya mizani katika utungo unaohusika.

2.3.1.8 Vina

Vina ni silabi zenye milio inayofanana. Katika tenzi za Kiswahili, kwa kawaida, vina huekwa mwishoni mwa msitari. Kazi kubwa ya vina ni kuongeza mvuto wa mlio wa Utendi, kumalizia misitari au vipande, kusisitiza maudhui na kurahisisha uhifadhi wa tungo hizo kichwani.

Maelezo hayo, ni muhimu sana katika uchunguzi huu, kwani, vipengele vya fani ni miongoni mwa vipengele ambavyo vilichunguzwa katika utafiti wetu, ili, kuona namna

vilivyotumika katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Mtafiti aliyatumia mawazo hayo, katika kuchunguza namna vipengele hivyo, vya kifani vinavyojidhihirisha katika Utendi wa Kiswahili.

2.3.2 Mtindo

Njogu na chimerah (1999), wanaeleza kuwa, mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwengine. Wanataalimu hawa wanaeleza kuwa, unapochunguzwa mtindo katika Utenzi, inapasa kuchunguza matumizi ya maneno yaliyotumika; iwapo maneno hayo ni maneno magumu, ya asili, na sababu za kutumia maneno hayo. Pia, inahitajika kuchunguza iwapo mtunzi amechanganya lugha. Mtindo katika ushairi, hutambulika kwa kuchunguza mishororo ya Utenzi na takiriri zilizojitokeza. Aidha, mtindo hutambulika kwa kuchunguza namna utungo huo ulivyoumbika. Hapa unachunguzwa utungo huo namna ulivyoanza, ulivyoendelezwa na ulivyomalizia.

Ingawa Njogu na Chimera hawakuonesha namna ya kuchambua vipengele hivyo, maelezo hayo yanayohusu namana ya kuchunguza mtindo wa Utenzi/Utendi yalimsaidia mtafiti katika kuchunguza na kuchambua data zinazohusiana na mtindo na hivyo, mawazo hayo yalisukuma mbele utafiti huu.

2.3.2.1 Uteuzi wa Maneno

Njogu na Chimera (1999), wanaeleza kwamba, mafanikio ya Utendi hutegemea namna mtunzi alivyomudu kuteua maneno na kuyapanga katika mpango unaofaa, ili, yalete athari aliyoikusudia mtunzi. Neno, huteuliwa kwa kutegemea kile kinachosemwa, muktadha wa kisarufi, sauti na umbo la shairi. Utenzi una mpangilio maalumu wa vina, maneno yanayoteuliwa, ni lazima yafuate mpangilio maalumu wa vina. Iwapo

maneno hayo ni marefu, inapasa yafupishwe, na iwapo maneno hayo, ni mafupi, itamlazimu mtunzi wa kazi ya Utendi ayarefushe. Mtafiti anakubaliana na mawazo hayo. Hivyo, mawazo hayo ya Njogu na Chimera yalichukuliwa kama ni muongozo wa kuchunguza namna uteuzi wa maneno ulivyojidhihirisha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*.

2.3.2.2 Mpangilio wa Maneno

Njogu na Chimera (1999), wameandika kwamba, maneno ya kazi za Utendi/Utenzi, hupangwa ili kuleta maana fulani, sauti za aina fulani, au urari fulani wa mizani. Hii ni kusema kuwa, Utendi/Utenzi humruhusu mtungaji, kukiuka kanuni za kisarufi, ili kuweza kuweka mizani na mfuatano unaokubaliana na mtiririko wa utungo wa kishairi. Katika kauli hiyo, mtafiti alipata mawazo yaliyomsukuma kuchunguza namna mpangilio wa maneno ulivyojidhihiisha katika tendi zilizofanyiwa utafiti.

2.3.2.3 Takiriri

Kutokana na ukweli kwamba, takriri ni mbinu inayotumika kwa kiasi kikubwa katika Utendi, mbinu hii imekuwa ikifanyiwa uchunguzi na watafiti wengi. Njogu na Chimera (1999), wanaeleza kwamba, takiriri ni mbinu ya kurudia rudia jambo, kwa kusudi maalumu. Katika Utendi, vina na urari wa mizani ni aina moja ya takriri. Pia mtunzi, anaweza kurudiarudia maneno au silabi, ili, kufikia madhumuni aliyoyakusudia.

Ndumbu (2013), alifanya uchunguzi uliohusu matumizi ya takiriri na sitiari katika Utenzi wa Rasi-lGhuli. Ingawa utafiti huu ulihusu Utenzi mwengine wa Kiswahili, kazi hiyo ilimsaidia mtafiti kusukuma mbele uchunguzi huu kwa kumbainishia namna ya kufanya uchunguzi wa takiriri na sitiari zinazojitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo* na namna vipengele hivyo vinavyochambuliwa.

2.3.2.4 Wizani

Wamitila (2008), anasema, wizani ni urari wa mapigo ya sauti katika kuongea. Utendi pia huwa na mahadhi ya kimazungumzo yanayofuata sauti, idadi ya silabi au pumzi ya msemaji.

Kutoka kwa mtaalamu huyu, tunajifunza kwamba, Utendi lazima ufuate kanuni ya wizani na taratibu zinazokubalika miongoni mwa Waswahili. Kazi ya Wamitila imesaidia kuona kwamba Utendi lazima ufuate kanuni husika na kwamba fani ya Utendi wa Waswahili, hauwezi kukiukwa. Kwa mfano;

14. Khafula kikutoke<u>ya</u>
Mkoyo hukutoke<u>ya</u>
Tapo ukakuwili<u>ya</u>
Ukutapo na kuli<u>ya</u>.

50. Liyongo akatambu<u>wa</u>
Huzengea kuua<u>wa</u>
Pale pate kayepu<u>wa</u>
Barani akitembeya.
(Kijumwa, 1913).

2.3.3 Matumizi ya Lugha katika Utendi

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), anaeleza kuwa, matumizi ya lugha katika Utenzi ni ya kipekee ukilinganisha na matumizi ya lugha katika tanzu nyengine. Kwa mfano, mtunzi wa UtenziUtendi ana uhuru mkubwa sana katika matumizi ya lugha, uteuzi wake wa msamiati, ubunifu wake, kubuni msamiati wake au maneno unde, kuyaendeleza maneno kwa njia tafauti. Utenzi unakawaida ya kutumia maneno ya kale. Pia, mtunzi ana uhuru wa kuipinduwa miundo ya sentensi au kisintaksia. Miundo hii inaweza kusababishwa na nia ya kupata upatanifu wa kiarudhi au sababu ya kibalagha. Unapogeuzwa muundo wa sentensi wa kawaida husisitiza kinachotangulia au kuja mwanzoni. Baadhi ya vipengele vya lugha vilivyofanyiwa uchunguzi katika tenzi teule ni kama vifuatavyo:

2.3.3.1 Taswira.

Taswira ni picha ya kitu au dhana fulani, katika ubongo wa msomaji au msikilizaji, kwa kutumia maneno. Picha ya maneno ikichorwa vizuri, mtu anaweza kuhisi, kuona, kuamini, kugusa , kuonja na hata kusikia.

Vipengele hivi vya kimtindo kama vilivyofafanuliwa vilikuwa na umuhimu sana katika kufikia khitimisho la madhumuni ya utafiti huu, kwani vipengele hivyo, ni miongoni mwa vipengele vya fani vilivyofanyiwa uchunguzi na mtafiti.

2.3.3.2 Maswala ya Balagha

Kwa mujibu wa Oyoyo (2013), anaeleza kuwa, maswala ya balagha ni mbinu ambayo hujitokeza katika fasihi, pale ambapo mtunzi au mhusika huuliza masuali kwa lengo la kumtanabahisha msomaji au msikilizaji. Masuala hayo huulizwa bila majibu. Dhima ya maswala ya balagha ni kutoa mawazo au hisia za ndania za mhusika au kuweka jambo wazi kwa hadhira na ambalo linahitaji kuangaziwa kwa umakini. Aidha, masuala ya balagha hutumiwa kusisitiza wazo ambalo mtunzi hakudhamiria kulieleza tu au kulitaja bayana. Ingawa kazi ya Oyoyo ilikuwa tafauti na kazi inayotafitiwa, hata hivyo, kazi hiyo, ilimsaidia mtafiti namna ya kuchunguza masuala ya balagha katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

2.3.3.3 Tabdila

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), anaeleza kuwa, tabdila ni mbinu ya kuliendeleza neno kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Mbinu hii hutumiwa sana katika Utendi/Utenzi kwa madhumuni ya kuwa na vina au mizani inayotakiwa. Msingi wa tabdila ni kubadili muundo uliozoeleka. Mawazo hayo ya Wamitila, yalimsaidia mtafiti kuona namna tabdila ilivyotumika katika maneno yaliyomo katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

2.3.3.4 Mazida

Wamitila (2008), anaeleza kuwa, mbinu ya mazida ni mbinu ya kurefusha, ambapo neno linaongezewa sauti ama silabi lakini bila ya kubadilisha maana yake. Aidha, maelezo haya yalimsaidia mtafiti, kutokana na kumpa msukumo wa kuyachunguza maneno ya tenzi teuliwa, ili kuona namna yalivyorefushwa na sababu ya huko kurefushwa.

2.3.3.5 Iksiri

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), iksiri ni mbinu ya kuyafupisha maneno kwa kuyadondosha sauti au silabi. Mawazo hayo, pia yalisukuma mbele utafiti huu. Kwa sababu, mtafiti alichunguza namna maneno yalivyofupishwa katika tenzi zilizotafitiwa.

2.3.3.6 Kinaya

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), kinaya ni tamathali ya usemi inayohusisha ukinzani kati ya hali ilivyo. Kinaya ni kauli ambayo ina maana ya kinyume. Kinaya katika Utenzi/Utendi hujitokeza kwa njia ya majibizano yanayoonesha kinyume cha matarajio au matumaini ya mhusika fulani. Kinaya huwa na pande mbili, upande wa msemaji na upande wa msikilizaji. Msemaji ana maana tafauti na anavyotarajia msikilizaji. Dhima kuu ya kinaya ni kuibua ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

2.3.3.7 Sitiari

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), sitiari ni tamathali ya ulinganishi bila ya kutumia viunganishi vya kulinganisha kama vile; “kama,” “ja,” `mfano wa`, na `mithili ya` Oyoyo (2013), TUKI (1984), wanasema kuwa, sitiari ni tamathali ya usemi inayohusisha vitu au viumbe viwili vilivyotafauti kitabia au kimaumbile kwa msingi wa sifa, iliyo katika vyote viwili, lakini, ulinganishi huo, haujitokezi wazi wazi, kwa sababu

ya kutatumia vilinganishi kama vile; `mfano`, `mithili`, `ja`. Matumizi ya sitiari hujenga picha fulani katika ubongo wa msikilizaji au msomaji.

2.3.3.8 Tashibiha

Tashibiha ni tamathali ya usemi ambayo hulinganisha vitu viwili ambavyo havihusiani kwa kutumia maneno kama vile: kama, mithili, kwamfano, sawa sawa (Njogu na Chimera, 1999). Mbinu hii inapotumika, msomaji au msikilizaji huweza kuchora taswira akilini mwake, jambo ambalo linarahisisha uelewaji wa kile kinachozungumzwa.

2.3.4 Wahusika

Chaligha (2013), Mulokozi (2002), wanasema, mhusika shujaa wa Kiafrika, sharti awe na msaada kwa watu wake. Mawazo hayo ingawa yalihusu kazi tafauti na inayotafitiwa, hata hivyo, yalikuwa na manufaa kwa mtafiti, kwani yalimsukuma mtafiti kuchunguza namna mhusika shujaa anavyohusishwa na watu wake na jamii kwa jumla.

2.3.5 Mandhari

Njogu na Chimerah (1999), mandhari yanahusu, wapi kazi hiyo ilitumiwa kijiografia, wakati wa kihistoria na inawahusu kina nani. Mandhari ni kipengele muhimu sana katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Sababu ya msingi ni kwamba, matukio katika kazi ya fasihi, na ubunifu unaojitokeza, hutegemea mahali na wakati. Wamitila (2002), anaeleza kuwa, mandhari ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini matukio yalifanyika. Anaongezea kusema kuwa, neno hili, hutufichulia wakati na sehemu matukio yalipotokea. Nafasi ya mandhari katika Utendi/Utenzi huwa ni uendelezwaji wa maudhui ya utungo huo. Kwa mfano, ikiwa Utenzi unawasilisha

masuala ya kijamii, sharti mandhari yawe bayana, ili, kutia uzito thabiti wa kile anachokielezea mtunzi wa kazi hiyo.

2.3.6 Kuhusu upekee wa Utendi/ Utenzi

Mukuthuria (2007), alifanya uchunguzi katika utungo wa *Sifa za Nguvumali,* ingawa pamekuwa na mjadala unaohusu utungo huo, kwa namna ulivyokiuka kanuni ya vina katika baadhi ya vina vya bahari ndogo, mizani zake katika baadhi ya misitari na hata tafauti ya idadi ya misiari kutoka ubeti mmoja na mwengine, hata hivyo, kazi hiyo, ilimsaidia mtafiti kuona namna ya kuchunguza upekee katika vipengele vya fani, kama wahusika, mtindo, muundo na mandhari. Ingawa kazi hiyo ili husu utungo mwengine, ilimsaidia kutambua namna ya kuchambua vipengele vya fani katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

Ouma (2013), alifanya utafiti wa kuchunguza maudhui teule yanayojitokeza katika Utenzi wa Nabii Issa (A.S). Maudhui aliyoyachunguza ni pamoja na ushujaa, dini, uislamu na ukafiri, malezi na nafasi ya mwanamke. Utafiti huo, ingawa ulihusu kuchunguza maudhui, hata hivyo, ulimsaidia mtafiti katika kufanya uchunguzi wa sifa za fani za Utendi wa Kiswahili. Kwa sababu, lengo la Ouma lilikuwa kuchunguza dhamira zilizojitokeza katika Utenzi wa Nabii Issa (A.S), kwa upande mwengine, alichambua vipengele vya fani vilivyojitokeza katika Utenzi huo, akieleza kuwa, hiyo ni mihimili ya kufikia khitimisho la uchunguzi wake. Kwa hivyo, mtafiti alipata ufahamu wa namna ya kuchunguza vipengele vya muundo na vya wahusika katika *Utendi wa Fumo Liyongo*.

Vile vile, Ndumbaro (2013), alichambua shujaa wa Epiki za Ulaya na kuchunguza shujaa wa tenzi za Kiswahili. Tenzi alizozishughulikia ni pamoja na *Utenzi wa Rasi-*

lGhuli, Utendi wa Mikidadi na Mayasa. Ndumbaro (Kashatajwa), alimnukuu Okpehwo (1976), akisema, shujaa wa Utendi wa Kiafrika, huonekana yuko peke yake.

2.3.7 Mapisi ya Fumo Liyongo

Mulokozi (1999), Njogu na Chimera (1999), wanaeleza kuwa, Fumo Liyongo ni shujaa, aliyewahi kuwapo katika eneo la Upwa wa Afrika Mashariki. Japo kuna utata kuhusu tarehe aliyozaliwa Liyongo, lakini, tarehe inayoelekea kukubalika zaidi, ni ile ya karne ya 13-14, kwa kuwa kitabu cha *Tarehe ya Pate* (Freeman-Grenville, 1996), kinamtaja mtawala wa eneo la Ozi, aitwaye Fumo Liyongo, aliyeishi wakati wa utawala wa Fumo Omar, mtawala wa ki-Nabhani, wa dola ya Pate. Inaelezwa kuwa, Fumo Omar, alitawala miaka ya 740-795 Hijiria, sawa na 1340-1393 M. Liyongo aliwahi kupigana na Fumo Omar.

Mulokozi (1999), anasema kuwa, Liyongo aliishi Pwani ya Kaskazini ya Kenya, kwenye maeneo ya Pate na Ozi, kwenye karne ya 14 au kabla. Mama yake aliitwa Somoa Mwana. Liyongo alikuwa kiongozi wa jamii yake, japo, hakuna uhakika wowote kuwa, alikuwa Mfalme. Pia, Fumo Liyongo alikuwa shujaa, manju wa ngoma, malenga na mwindaji hodari. Liyongo alikuwa akifanya biashara na kuwinda sehemu za bara karibu na Pate. Liyongo aliweka makaazi yake Ozi, na alikufa na kuzikwa Kipini, mahali paitwapo, Ungwana wa Mashaha.

2.4 Uchaguzi wa nadharia

Kwa mujibu wa Sengo (2009), Nadharia ni wazo kuu, fikira kuu, muongozo mkuu wa mtu au wa jamii, wa pahala na, wa wakati. Mtafiti wa kazi hii ameongozwa na Nadhariaya Umuundo na Nadhariaya Ujumi wa Kiafrika ili kufikia lengo lake.

2.4.1 Nadharia ya Umuundo

Wamitila (2002), muasisi wa Nadhariaya Umuundo ni Ferdinand de Saussure. Nadhariaya umuundo, inaangalia na kuipa umuhimu fani, katika kazi ya sanaa. Wana Umuundo, wanaeleza kuwa, mbinu za kisanaa zilizosukika vizuri, ukiwamo ufundi wa kutumia lugha, ndiyo kitu muhimu katika kujenga kazi ya fasihi. Dhana ya umuundo, inaangalia na kuipa umuhimu fani, katika kazi ya sanaa. Kazi ya fasihi, iweze kuwa tafauti na kazi nyengine zisizokuwa za fasihi. Kwa hiyo, katika muundo, inazingatiwa jinsi lugha inavyotumika. Nadharia hii, pamoja na kuwa, ina upungufu kwa kuipendelea zaidi fani kuliko maudhui, katika kazi za fasihi, mtafiti aliitumia kuchunguza sifa za muundo wa Utendi/Utenzi wa Kiswahili, ili kuona namana sifa za kipekee za kifani zinavyojidhihirisha katika tendi za Kiswahili.

2.4.2 Nadhariaya Ujumi wa Kiafrika

Njogu na Wafula (2007), wanaeleza kuwa, Nadhariaya Ujumi, iliasisiwa na Pio Zirimu (1971). Sengo (1999), katika kazi ya fasihi, ujumi una maana ya ladha tamu au chungu – ya kazi ya fasihi. Ujumi ndiyo unaomfanya msomaji kuisoma, si mara moja wala mbili, bali kila akimaliza, hupenda aisome tena na tena. Njogu na Wamitila (2007), wanaeleza kuwa, Wazungu walipokuja katika bara la Afrika, walianzisha matusi na kashfa nyingi. Wazungu walimuona Muafrika kuwa ni mshenzi na asiyejua chochote. Hivyo, Nadharia hii, ina lengo kuu la kuirudisha na kuielezea hadhi ya Muafrika kisawasawa.

Uafrika uelezwe vizuri na watu wote, weusi kwa weupe, mashujaa wa Afrika waoneshwe katika kazi za fasihi na utumiaji wa lugha za kiafrika katika uandishi wa kazi za fasihi. Pia, Nadhariahii, inatilia mkazo matumizi ya mbinu zinazofungamana na

Uafrika au mazingira ya Kiafrika katika kazi za fasihi. Kwa mfano; mibuyu, mikuyu, istiara, tambiko za Kiafrika, maudhui ya Kiafrika na tanzu za fasihi ya Kiafrika.

Nadhariahii ya Ujumi na Nadhariaya Umuundo, zilichaguliwa na mtafiti, kumuwezesha kuchunguza sifa za fani za *Utendi wa Fumo Liyongo*.

2.5 Hitimisho

Sura hii ilialezea machapisho ambayo mtafit aliyatalii na kumpatia uelewa wa kina juu ya kile kilichotafitiwa. Pia, utafiti umemalizia kwa kuzielezea nadharia za ujimi wa Kiafrika na nadharia ya umundo ambazo zilimuongoza mtafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti kukusanya na kuchambua data zitakazomuwezesha kufikia lengo la utafiti husika (Enon, 1998).

3.1 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti la kijiografia ni pahala ambapo mtafiti alikwenda kukusanya data. Hivyo, utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, tawi la Pemba, Maktaba kuu Pemba, na maktaba ya Skuli ya Fidel Castro. Maeneo hayo yalichaguliwa na mtafiti kwa sababu, utafiti huu ni utafiti wa Maktabani, na kwa sababu utafiti huu ulifanyika wakati shule ziko wazi. Kwa vile, mtafiti ni muajiriwa hakuwa na muda wa kwenda nje ya Kisiwa cha Pemba kutafuta data.

3.2 Uteuzi wa Data

Uteuzi ni kitendo cha kuchaguwa au kupata kikundi kiwakilishi kinachoitwa kundi lengwa. Utafiti huu ulitumia uteuzi lengwa. Kwa mujibu wa Enon (1998), anaeleza kuwa, uteuzi lengwa ni ule wa mtafiti wa kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazozihitaji. Mtafiti alitalii tenzi za Kiswahili, na kuchagua *Utendi wa Fumo Liyongo.* Aliona Utenzi huo, utajibu maswali ya utafiti huu.

3.3 Wateuliwa

Wateuliwa katka utafiti huu ni watu au vitu vilioteuliwa, kiuwakilishi, jamii kuu ya utafiti, kujibu masuali ya utafiti (Enon, 1998). Katika utafiti huu, *Utendi wa Fumo Liyongo* uliteuliwa na mtafiti, ikiwa kazi teule. Mtafiti aliuteuwa *Utendi wa Fumo*

Liyongo kwa sababu, ni miongoni mwa tenzi ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kina wa sifa za kifani.

3.4 Mbinu za Kukusanya Data

Ukusanyaji wa data, hutumia njia ya Maskanini ama Maktabani. Ukusanyaji wa data za Maskanini, hutumia mbinu za dodoso, usaili na uchunguzi. Njia ya Maktabani hutumia mbinu kama vile; usomaji wa makala, majarida, vitabu, tasnifu, magazeti na wavupepe. Enon (1998), anaeleza kuwa, dhana ya ukusanyaji wa data, ni zoezi la awali katika utafiti, zoezi ambalo, humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika lengo lake la utafiti. Aidha, hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanyaji wa data.

3.4.1 Mbinu ya Usomaji Maluii

Mbinu ya usomaji makini ni mbinu inayohusu utalii wa kina wa kazi zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusiana na mada ya utafiti. Kazi hizo, aghalabu zinahusu nadharia za utafiti na uchambuzi wa dhana (Enon, 1998). Mbinu ya Maktabani, ilitumika kwa kusoma makala, vitabu, na tasnifu ili, kuchunguza namna vipengele vya fani vilivyojitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo.* Mtafiti alitumia mbinu hii na ilimuwezesha mtafiti kupata data za utafiti huu, na kufikia madhumuni ya utafiti wake.

3.5 Vifaa vya Utafiti

Mulokozi (1983), anaeleza kuwa, vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivyo huwa ni pamoja na; kalamu na karatasi, shajara ya Masikanini, tepu rekoda (kirimbo) na vifaa vyake, video (pataninga); na vifaa vyake, kamera na vifaa vyake, ngamizi na vikorokoro vyake, hojaji, vifaa vya kupimia na kuhesabia. Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni;

Kalamu na karatasi: kwa ajili ya kuandikia data za utafiti

Wavupepe: kwa ajili ya kutafutia machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti huu.

Majarida: kwa ajili ya kutalii marejeleo yanayohusiana na mada ya utafiti huu.

3.6 Hitimisho

Sura hii inaelezea mbinu zilizotumika kukuwaji data na kuzichambua. Sura imeelezea utenzi wa data, mbinu ya uteuzi wa data ambayo imeelezwa kuwa ilitumika mbinu ya uteuzi tengwa. Pia, data zilikusanywa kwa mbinu ya utenzi makini. Sura inamalizi kwa kuelezea vifaa vya utafiti.

SURA YA NNE

UCHAMBUZI WA DATA

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, data zilizokusanywa na mtafiti zimefanyiwa uchambuzi kutegemea madhumuni maalumu ya mtafiti. Pia, sura hii imeelezea sifa za *Utendi wa Fumo Liyongo.* Aidha, sehemu hii imeelezea vipengele vya fani vinavyojitokeza katika*Utendi wa Fumo Liyongo*, vipengele hvyo, vimejumuisha; wahusika, muundo, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha. Sura imemalizia kwa kuchambua data zinazoonesha upekee wa*Utendi wa Fumo Liyongo*.

4.1 Uchambuzi wa Data

Mtafiti alitumia mbinu ya Makatabani kukusanya data, ambazo alizipata kutoka katika *Utendi wa Fumo Liyongo.* Data zilizokusanywa na mtafiti zilifanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kutegemea madhumuni mahususi. Data hizo zilifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo;

Jadweli 2. Sifa za Utendi/Utenzi wa Kiswahili.

Na.	**SIFA YA UTENDI/UTENZI WA KISWAHILI**
1	Muundo wa Ushairi uliyo katika bahari ya Utendi
2	Wingi wa beti
3	Sifa ya kuwapo au kutokuwapo mhusika shujaa
4	Kunapatikana mapisi

5	Mianzo na miishio ya kifomula
6	Maudhui ya kidini kwa kiwango kikubwa
7	Uunganifu

4.1.1 Bahari ya Utendi

Kwa mujibu wa data zilizo kusanywa na mtafiti, imebainika kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo* una sifa ya muundo na mtindo wa ushairi unaofuata bahari ya Utendi. *Utendi wa Fumo Liyongo*, umetumia bahari ndogo "ya" kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Beti chache tu ndizo zilizokiuka kanuni hiyo. Beti hizo ni beti za 17 na 30, zimeishia "a" na "wa." *Utendi wa Fumo Liyongo*, kama, ilivyo kaida ya bahari ya Utendi, umejengeka kwa; misitari mine, katika kila beti. Misitari hiyo, ina kipande kimoja kimoja. Kila kipande, kina mizani nane nane. Kwa mfano:

35. Ruhu zikenda kishi**ndo**
Zimo zao hukoma o<u>ndo</u>
Huyo ni bwana wa ko<u>ndo</u>
Ashindaye jeshi ni<u>ya.</u>
(Kijumwa, 1913)

Vile vile, *Utendi wa Fumo Liyongo*, una kina kinachobadilika kutoka beti moja na nyengine. Kwa mfano, katika mfano hapo juu, silabi "**ndo**" imerudiwa rudiwa katika msitari wa pili na wa tatu. Hali hii imejidhihirisha katika beti zote za *Utendi wa Fumo Liyongo*

4.1.2 Mianzo na Miisho ya Kifomula

Mtafiti amegunduwa kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo*, unatumia mianzo maalumu na kumalizia kwa miisho maalumu. Utendi huo umeanza kwa duwa na kumalizia kwa duwa. Duwa hiyo, anaombwa Mwenyezi Mungu Mmoja, ambaye ndiye Mwenye uwezo wa kila kitu. Aidha, katika duwa hizo, ametajwa Mtume Muhammad (S .A .W), ambaye

ndiye Mtume wa mwanzo na wa mwisho katika ulimwengu huu. Kwa mfano, *Utendi wa Fumo Liyongo*, ubeti wa kwanza, kuna duwa:

1. Bismillahi nabutadi
   Kwa ina la Muhammadi
   Nandikie auladi
   Nyuma watakaokuya

Kutokana na ubeti huo wa kwanza, *Utendi wa Fumo Liyongo*, mtunzi anaanza jina tukufu la Bismilahi, kisha, anamtaja Mtume Muhmmad (S.A.W). Hii ni dasturi ya waumini wa Dini ya Kiislamu, ambapo, kila jambo, hulianza kwa mtajo wa Allah (S.W), yaani `Bismi Llahi Rahmani Rahimi`.

Vile vile, katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, mtunzi anamalizia kwa kumuomba Mwenyezi Mungu (S.W), katika ubeti wa 228 na wa 229, ili akirimiwe, na AIlah (Mwenyezi Mungu). Mfano;

228. Tumeziya kukhitimu
     Hapo ndio wasalamu
     Ilahi tatukirimu
     Kwa Baraka na afiya

229. Rabbi tatusahiliya
     Na uzito wa duniya
     Tena tatujaaliya
     Kuwa njema yote niya

Katika mifano hiyo hapo juu, mtunzi anamuomba Mwenyezi Mungu, Amuepushie uzito wa dunia. Pia, anamuomba Mola, Aifanye vyema niya yake. Mwenyezi Mungu, Ameoneshwa kuwa, ndiye Mwenye uwezo wa kila jambo kwa mja wake.

4.1.3 Uunganifu

Ndumbaro (2013), anaeleza kuwa, sifa ya Utendi uuganifu, ni sifa ya Utendi wenye msuko na mfuatano wa kimantiki wa visa. Mtafiti amegunduwa kwamba, *Utendi wa*

Fumo Liyongo, una Uunganifu wa visa na mtiririko wa visa vyenye mantiki ambapo, Utendi huo, unaanza kwa kutusimuliya kubalekhe kwa Liyongo, namna alivyotakiwa na Mfalme, kufika Pate. Baadaye, unatusimuliya namna Mfalme, alivyoingia khofu ya kunyang`anywa ufalme. Kutokana na hali hiyo, Mfalme aliamua, kumtegea mitego Fumo Liyongo, ili amnase. Mfalme alifanikiwa kumtia gerezani Fumo Liyongo, ambako, baadaye alifanikiwa kutoroka.

Baada ya kushindwa kwa njama hiyo, Mfalme aliamua kumtumia mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo, ili kugunduwa siri ya kile kilichoweza kumuua. Mtoto huyo wa kambo wa Fumo Liyongo, alikubali kugunduwa siri hiyo. Baada ya kufanikiwa kuipata siri, mtoto huyo, alirudi kwa Mfalme na alipewa sindano ya shaba. Mtoto alifanikisha kifo cha Fumo Liyongo. Mfalme alipopata taarifa ya kifo cha Fumo Liyongo, alimfukuza mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo. Baada ya muda mfupi, mtoto naye alipata ugonjwa na kufariki. Hivyo, masimulizi hayo, yameungana toka mwanzo hadi mwisho wa Utendi huo. Hata hivyo, ni vyema kuikwa wazi kuwa, masimulizi yanayoonesha uunganifu wa *Utendi wa Fumo Liyongo*, yamefuata bahari ya Utendi.

4.1.4 Wingi wa Beti

Suala la wingi wa beti katika Utendi/Utenzi, limezua mjadala mrefu miongoni mwa watafiti. Mulokozi (1999), anasema bado kuna utata juu ya tendi kuwa na urefu wa kutosha. Sababu kubwa ni kwamba haujuilikani huo urefu wa kutosha ni upi?

Mtafiti alizikusanya data, na kuzichambua na kugunduwa kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo* una jumla ya beti 232, ambazo zimekamilisha masimulizi ya shujaa Fumo Liyongo na mpinzani wake, Mfalme wa Pate. Ukamilifu huo wa masimulizi ya kisa cha Liyongo ndiyo unaojenga Utendi wenyewe.

4.1.5 Kielezea cha Kuwapo au kutakuwapo kwa Shujaa.

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo* data zimeonesha kuwa, kuna mhusika shujaa Fumo Liyongo. Shujaa huyo anahusishwa na Ushujaa wa nguvu za kimwili, ujasiri na uwezo wa kiakili. Kwa upande wa nguvu za kimwili, Fumo Liyongo alikuwa na uwezo wa kuwakabili watu mia na kuwashinda. Kwa mfano;

12. Mfalume kawambiya
    Wagala kiwasifiya
    Huwegema watu miya
    Wasiweze kukimbiya

Aidha, kutokana na nguvu alizokuwa nazo, Fumo Liyongo, alifananishwa na simba. Katika Ubeti wa 12-15, Liyongo aliweza kuwaegemea watu mia na hawakuweza kusitahamili. Fumo Liyongo alikuwa kama simba. Alipowatokea watu, mikojo iliwatoka na walilia. Watu aliowatolea macho tu, waliweza kuzimia kwa khofu.

15. Mato kikukodoleya
    Ghafula utazimiya
    Kufa kutakurubiya
    Kwa khaufu kukungiya.

Vile vile, Fumo Liyongo aliweza kubeba mizigo iliyojaa chumba kizima. Hali hii si ya kawaida kwa binaadamu wa kawaida. Katika beti za 37-39 tunasimuliwa namna Fumo Liyongo alivyochukua vitu vilivyojaa chumba kizima. Kwa mfano;

37. Kisa katiti kutuwa
    Mkobani akatowa
    Zitu alizotukuwa
    Nyumba ndima nisikiya.

Nguvu nyengine alizokuwa nazo Fumo Liyongo, zinadhihirika pale alipopuliza panda na kupasuka kutokana na nguvu za pumzi alizokuwa nazo, beti za 27-31.

27. Liyongo kenda muini
    Akipata mlangoni

Panda katia kanwani
Kivuzia kapasua.

Fumo Liyongo, aliweza kutembea umbali wa kwenda siku nne, kwa kutumia muda wa siku mbili tu. Uwezo huo, unaelezwa wakati Fumo Liyongo, alipofunga safari kutoka Shaka kuelekea Pate. Ubeti wa 25 na 26 unatusimulia habari hiyo,

25. Na mtu kitoka Shaka
Hata Pate ukafika
Siku nne kwa haraka
Alo hodari sikiya.

26. Liyongo akikabili
Ndiya kenenda rijali
Alikwenda siku mbili
Na ya pili ni kungiya,

4.1.6 Mapisi katika Utendi wa Fumo Liyongo

Mtafiiti, baada ya kuchambua data alizozikusanya kutoka *Utendi wa Fumo Liyongo* amegunduwa kwamba, Utendi huo umebeba mapisi katika vipengele vilivyofanyiwa uchambuzi, na mtafiti kama ifuatavyo:

4.1.6.1 Mapisi ya mhusika Fumo Liyongo

Mtafiti amegunduwa kuwapo mapisi katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Tunaelezwa kwa ufupi, mapisi ya mhusika Fumo Liyongo na maisha yake kwa jumla. Fumo Liyongo alizawa Siu, Pate. Alifariki sehemu ya Mwana,

230. Ya Liyongo hukwambia
Siu alikozaliwa
Pate akitembeleya
Kwa Mwana akafiliya.

Wazo hilo, linakubalika kuwa, hiyo ni historia ya kweli inayomuhusu Fumo Liyongo. Utafiti unaonesha sehemu zilizotajwa katika ubeti wa 230, za *Utendi wa Fumo Liyongo* ndizo alizowahi kuishi Fumo Liyongo.

Aidha, Mulokozi (1999), anaeleza kuwa, Fumo Liyongo alikuwa ni manju wa nyimbo, katika taalimu ya Fasihi ya Kiswahili. Hadi leo, zipo kazi ambazo zimetafitiwa na kukusanywa, ambazo zinaaminika zilitungwa na Fumo Liyongo.

Aidha, katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, tunasimuliwa umanju aliyokuwa nao Fumo Liyongo. Wakati Liyongo, alipokuwa katika gereza, aliomba apigiwe ngoma. Hiyo, ilikuwa ni njama, ili, kufanikisha mpango wake; hiyo ilikuwa ni kawaida yake. katika ubeti wa 98, tunaelezwa;

98. Akajibu "Usikhini
Kamwambie Sulutwani
Mwao nimeutamani
Na gungu liwe pamoya

Pia, mapisi yanayoonesha umanju wa mhusika Fumo Liyongo, yanajidhihirisha wakati alipokuwa gerezani. Tunaelezwa kuwa, Fumo Liyongo alimpa ujumbe Sada, ampelekee mama yake kwa njia ya Utendi/Utenzi. Mulokozi (1999), wakati akikusanya *Utendi wa Fumo Liyongo*, alikusanya wimbo huo wenye jumla ya mishororo 13, na kuuambatanisha mwishoni mwa Utenzi huo. Katika beti za 103-105, ni ufupishi wa wimbo huo;

103. Kanena kwa ushairi
"Enenda kamukhubiri
Mama afanye tayari
Haya nimezo kwambiya.

Aidha, tunaelezwa kwamba, Fumo Liyongo alikuwapo katika karne ya 13 au kabla. Fumo Liyongo aliishi pamaoja na Mfalme Fumo Omar, katika eneo la Pate (Mulokozi, 1999).

Mgogoro uliyokuwapo kati ya Fumo Liyongo na Fumo Omar, umeelezwa kwa kina katika Utendi huo. Tunaelezwa kwamba, Mfalme huyo, alijenga uwadui kati yake na Fumo Liyongo;

49. Fitina zikamngiya
Mfalume miya miya
Kwa hila kakusudiya
Kumuuwa fahamiya.

4.1.7 Dini katika Utendi wa Fumo Liyongo

Data zinaonesha kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo* umebeba maudhui ya dini ya Kiislamu. Utendi huo unaanza kwa mtunzi kuomba duwa kwa Mweyezi Mungu mmoja na kumaliza kwa duwa. Mtume Muhammad (S.A.W), pia anasifiwa katika utendi huo. Kwa mfano;

1. Bismillahi nabutadi
Kwa ina la Muhammadi
Nandikie auladi
Nyuma watakaokuya

Pia, Utendi wa Fumo Liyongo unamaliza kwa maombi;

228. Tumeziya kukhitimu
Hapo ndio wasalamu
Ilahi tatukirimu
Kwa Baraka na afiya

229. Rabbi tatusahiliya
Na uzito wa duniya
Tena tatujaaliya
Kuwa njema yote niya

4.2 Fani katika Utendi wa Fumo Liyongo

Fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira, Mbatiah (2001), Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999). Wamitila (2003), anaeleza kuwa, fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi ya kifasihi. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Hivyo, katika utafiti huu, vipengele vya fani vilivyofanyiwa uchunguzi ni vile vinavyohusiana na mandhari, wahusika, lugha, mtindo na muundo.

Mtafiti alikusanya data na kuzichambua na kugunduwa kwamba, *Utendi wa Fumo Liyongo*, umetumia vipengele vya fani vinavyoelezwa hapo chini;

4.2.1 Mandhari

4.2.1.1 Mandhari katika Utendi wa Fumo Liyongo

Utendi wa Fumo Liyongo, unayachora maisha ya jamii ya Pate ya wakati huo. Mandhari ya Utendi huo, ni mandhari halisi ya eneo la Upwa wa Afrika Mashariki, sehemu ambayo ni miongoni mwa makaazi ya Waswahili. Mandhari yanayojitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, ni mandhari yakinifu, yaliyofanywa uchambuzi kama ifuatavyo;

4.2.1.2 Mandhari ya gerezani

Gerezani ni moja kati ya mandhari yaliyotumika katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Gerezani aliwekwa Fumo Liyongo, ili, kudhibitiwa na Mfalme wa Pate. Katika gereza hilo, kulikuwa na askari, ambao walipewa kazi ya kumlinda Fumo Liyongo. Pia, waliendeleza dhuluma, kwa kuwanyan`ganya vyakula, wale wanaoletewa vyakula na jamaa zao. Katika ubeti wa 102, inaelezewa hali hiyo ya gerezani kama ifuatavyo;

102. Chakula wakimweteya
Asikari huiliya
Siku hiyo kamwambiya
Mamangu nisalimiya

Dhuluma hizo zimekuwa zikifanywa na vyombo vya dola kwa kutumia mwavuli wa jeshi. Hali hii, ndiyo, Mfalme aliiendeleza, ili, kudhibiti utawala wake dhidi ya wapinzani wake, akiwamo, Fumo Liyongo.

Huko gerezani Fumo Liyongo, alikuwa amefungwa kwa minyororo, ili kumdhibiti kizuizini. Katika ubeti wa 115, *Utendi wa Fumo Liyongo*, unathibitisha namna Fumo Liyongo alivyokuwa amedhibitiwa kwa kutumia minyororo;

115. Kulla nyimbo zizidipo
Na ngoma zitakatapo
Alikizitinda hapo
Pingu na minyoo piya.

Baada ya tukio la kuingizwa gerezani, Fumo Liyongo, alitakiwa auawe. Fumo Liyongo aliomba, apatiwa fursa ya kupigiwa ngoma kabla ya kifo chake. Hivyo, Fumo Liyongo;

98. Akajibu "Usikhini
Kamwambie Sulutwani
Mwao nimeutamani
Na gungu liwe pamoya"

Maombi hayo yalipokubaliwa na Mfalme, Liyongo alipata fursa ya kumtuma Sada akamwambie mama yake, amfanyie mkate mwema na ndani yake atiye tupa. Inaelezwa kuwa, ujumbe aliopewa Sada, ulikuwa katika mtindo wa ushairi. beti za 103-106, zinatubainishia tukio hilo kama ifuatavyo;

103. Kanena kwa ushairi
'Enenda kamukhubiri
Mama afanye tayari
Haya nimezokwambiya"

104. Kamba "Sada nakutuma,
Enda kamwambie mama
Afanye mkate mwema
Kati tupa aitiya"

Baada ya kufanikiwa kupatiwa tupa, iliyotiwa ndani ya mkate wa wisha, Fumo Liyongo alifanikiwa kujitowa gerezani kwa kuikereza minyororo aliyofungiwa na kuchupa dirishani.

4.2.1.3 Nyumbani kwa Mfalme

Kwa upande mwengine, mtafiti aligunduwa, kuna mandhari ya nyumba ya Mfalme yaliyotmika. Katika Utenzi huo, inaelezwa kuwa, Mfalme aliitumia nyumba yake, ili, kupanga mikakati na njama ya kumkamata Fumo Liyongo. Beti 123-129 zina bainisha hilo kama ifuatavyo:

124. Kapanda wakaonana
Pamoya na ule Bwana
Sulutwani akanena
Nakuomba yambo moya

126 Kwa baba enda sikhini
Umuulize yakini
Kimuuwacho ni n`ni
Nakuomba hili moya

Ubeti huu unaonesha jinsi, Mfalme huyo, alivyokuwa akitumia nafasi ya uongozi aliyokuwanayo, kufanikishia njama alizozikusudia. Mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo, alikubali kutimiza matakwa ya Mfalme, kutokana na kukhadaiwa.

124. Kapanda wakaonana
Pamoya na ule Bwana
Sulutwani akanena
`Nakuomba yambo moya`

126. `Kwa baba enda sikhini
Umuulize yakini
Kimuuwacho n`ni
Nakuomba hili moya`

127. Au wewe wakiyuwa
Nambiya sifaye tuwa
Uwaziri utapowa
Takuoza bintiya.

4.2.1.4 Mandhari ya Nyikani

Nyikani ni porini. *Utendi wa Fumo Liyongo,* umetumia mandhari ya Nyikani, ambako alikimbilia Fumo Liyongo. Kutokana na uwadui wa Mfalme wa Pate, inaelezwa kuwa, Mfalme hakuwa radhi, mpaka alipohakikisha amemmaliza Fumo Liyongo.

Mfalme alifanya njama ya kumuhadaa mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo, ili amfuate baba yake huko huko nyikani, ambako, inaelezwa katika ubeti wa 143 kuwa, mtoto huyo, alifanikiwa kupata siri ya kile, kilichoweza kumuuwa Fumo Liyongo na katika ubeti wa 179, inaelezwa namna mtoto alivyofanikiwa kumuuwa baba yake kutokana na ushawishi wa Mfalme;

143. Nisikiya wangu baba
Liniuwalo ni haba
Ni msumari wa shaba
Kitovuni nikitiya

179. Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t`ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya

Mtoto wa Fumo Liyongo, anawakilisha tabaka lililodanganywa, ili, kufanikisha matakwa ya Mfalme. Hayo, yalikuwako, siku za Manabii, Maswahaba na yapo, hadi leo, katika maisha khalisi.

4.2.1.5 Mandhari ya Mji wa Pate

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mandhari khalisi ya Pate. Ndani ya Utendi huo, mnatajwa jina khalisi la mji wa Pate, eneo lililopo Kaskazini mwa eneo la Waswahili;:

71. Mwambieni, `tusafiri
Hata Pate tukajiri
Hapana tena khatari
Habari tumesikiya`.

Mandhari hayo, yanathibitishwa na Utendi, ambamo, kumetajwa mijiti, kama vile; “mikoma”, ambayo imekuwa ikipatikana katika maeneo ya Pate. Kwa mfano, masimulizi hayo, yanapatikana pale Fumo Liyongo alipoandamana na Wagala, ili kwenda kuangua makoma.

Kwa mfano:

61. Liyongo kanena hima,
Uzengeeni mkoma,

Muyapendao makoma
Nipate kuwanguliya.

Pia, matumizi ya mhusika, *Mfalme*, yanadokezea kipindi cha kale, ambapo katika mwambao wa Afrika mashariki, kulitawala wafalme. Mandhari hayo, yanaelezea mapisi ya eneo la Upwa wa Afrika Mashariki na hali ya utawala uliyokuwapo.

4.3 Wahusika katika *Utendi wa Fumo Liyongo*

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, kuna wahusika, wanaotoka matabaka tafauti tafauti. Wahusika hao ni pamoja na Liyongo, Mama yake Liyongo, Sultwani, Wagala na mtoto wa kambo wa Liyongo.

4.3.1 Fumo Liyongo

Fumo Liyongo ndiye mhusika shujaa katika Utendi huo. Fumo Liyongo, anaelezwa alikuwa na nguvu za kuwakabili watu miya, na kuwashinda. Umbo lake lilifananishwa na lile la simba;

12. Mfalume kawambiya,
Wagala kiwasifiya,
“huwegemea watu miya,
Wasiweze hukimbiya.

13. Ni mwanamume Swahili,
Kama simba unazihi,
Usiku na asubuhi,
Kutembea ni mamoya.

Beti hizi, za 12 na 13 zinadhihirishia jinsi, mhusika huyo, alivyokuwa shujaa. Vile vile, katika ubeti wa 37-39 Liyongo alikuwa na nguvu za ajabu. Aliweza kubeba mizigo ya kujaza chumba kizima. Mtunzi wa Utendi huo, ametia chuku, ili, kusisitiza na kuonesha namna Fumo Liyongo, alivyokuwa na nguvu zisizokuwa za kawaida;

37. Kisa katiti kutuwa,
Mkobani akatowa,
Zitu alizotukuwa,
Nyumba ndima nisikiya.

Aidha, katika beti za 27-31, mnaelezwa, jinsi Liyongo, alivyoweza kulipuliza panda na kulipasuwa kutokana na nguvu alizokuwa nazo. Liyongo aliweza kutembea umbali wa mwendo wa siku nne kwa siku mbili, umbali ambao, watu wengine, kwa kawaida, walilazimika kutembea kwa siku nne kamili;

27. Liyongo kenda muini

Akipata mlangoni
Panda katia kanwani
Kivuzia kapasuya.

25. Na mtu kitoka Shaka,
Hata Pate ukafika,
Siku nne kwa haraka,
Alo hodari sikiya.

26. Liyongo akikabili,
Ndiya kenenda rijali,
Alikwenda siku mbili,
Na ya pili ni kungiya.

Vile vile, imegundulika kwamba, Liyongo ni mhusika aliyependwa na watu wa jamii yake. Kutokana na umaarufu wake, mwisho Sultwani wa Pate alimuwinda kwa kuwatuma Wagala, wamuue. Njama hizo, ziligonga mwamba, mwishoni Liyongo anazigunduwa njama hizo, za Sultwani. Khatimaye, Sultwani alifanikiwa kumtiya gerezani Fumo Liyongo;

91. Kiuwawa ndiyo sana
Kitouwawa ni zana
Hayo yot`e wakanena
Sulutwani kaambiwa

Katika ubeti wa 225, mumeelezewa kuwa, Liyongo alikuwa akipendwa sana na wanajamii. Baada ya kifo chake, inaelezwa namna watu walivyokuwa na huzuni kutokana na kumkosa kipenzi chao;

225. Liyongo silaha yetu
Kwa wut`e khasimu zetu
Alikuwa ngao yetu!
Wut`e wakinena haya.

Mbali na ushujaa na kupendwa na watu, Fumo Liyongo, kwa upande mwengine, katika ubeti wa 91, mnaelezwa, namna, Sultwani alivyoazimia kuwa, lazima Liyongo auawe;

91. `Kiuwawa ndio sana
Kitouwawa ni zana`
Hayo yot`e wakanena
Sulutwani kawambia

92. Sulutwani kafikiri
Kumuuwa ndio kheri
Kumuwata ni khatari
Kwa hila t`aizengeya

Liyongo alitiwa jela na Mfalme ili auawe. Katika ubeti wa 81, mumeelezewa njama alizozifanya Sultwani, ili, kuhakikisha anamkamata Liyongo. Iinatumiwa njama ya kualikwa Liyongo, kuhudhuria karamu ili auwawe.

81. `Kwa wanaume na wake,
Na Liyongo, mumwalike
Naadhimu nimshike
Ni siri nimewambiya.

Mfalme alifanikiwa kumuingiza Liyongo gerezani. Hata hivyo, kutokana na msaada wa mama yake na kijakazi Sada, anafanikiwa kutoka gerezani kwa kutumiya tupa aliyopelekewa na mama yake;

104. Kamba, “Sada nakutuma
Enda kamwambie mama
Afanye mkate mwema
Kati tupa aitiya.

117. Wakiinuka kuteza
Liyongo akatokeza
Khaufu ziliwakaza
Mbiyo zikawapoteya.

Liyongo baada ya kufanikiwa kutoka gerezani, alikimbiliya nyikani ambako alikwenda kuishi peke yake. Huko Liyongo alitowa siri kwa mtoto wake wa kambo, ambaye alighilibiwa na Sultwani. Mtoto huyo, alifanikiwa kumuuwa Fumo Liyongo kwa kumchoma sindano ya shaba kitovuni;

136. Babake akamwambiya
"Wewe kuuliza haya
Dhana nimekudhaniya
Kuniuwa huzengeya".

179. Kimtiya kitovuni
Naye ulele kwa t`ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya.

4.3.2 Sultwani

Sultwani alikuwa mtawala wa Pate. Mwanzo alikuwa na mapenzi na Fumo Liyongo. Hata hivyo, mwisho alijenga uwaduwi mkubwa juu ya Fumo Liyongo. Mtawala huyo, ndiye aliyefanya kila hila, ili aumuuwe Liyongo;

207. Mfalume kipulika
Liyongo ametoweka
Nde mui meanguka
Haya aliazimia.

Mfalme huyo alikuwa ni muuwaji.

49. Fitina zikamngiya
Mfalume miya miya
Kwa hila kakusudiya
Kumuuwa fahamiya.

4.3.3 Mama yake Liyongo

Mama wa Liyongo, ndiye aliyekuwa akimsikiliza sana. Alimhudumia kwa kumpelekea chakula wakati alipokuwa kifungoni. Mama huyo, ndiye aliyefanikisha kumtowa kifungoni Liyongo, kwa kumpelekea tupa, Fumo Liyongo. Maamuzi hayo, aliyafanya baada ya kupata maagizo kutoka kwa Liyongo kwamba atengeneze mkate na kati atiye tupa na alifanya hivyo;

110. Mama tupa akitiya
Kitambaa metatiya
Kwa furaha mno ghaya
Sana kawafurahiya.

Mtafiti amegunduwa kuwa, huyo ni mhusika ambaye anamsaidia mtoto wake, ili, kujitoa katika matatizo yaliyomkabili. Shujaa wa tenzi huu, anapata msaada kutoka kwa watu wake wa karibu.

4.3.4 Mtoto wa Kambo wa Liyongo

Mtoto wa kambo wa Liyongo alikuwa ni msaliti, kwa kukubali kuhadaiwa na Mfalme, ili, amuuwe babaake. Anapewa ahadi ya kupewa mali, ikiwamo kujengewa nyumba na kuozeshwa mtoto wa Mfalme, hata hivyo, baada ya kufanikisha matakwa ya Mfalme, ya kumuuwa Liyongo, Mfalme anamfurusha mtoto huyo kwa sababu ya kukhofiwa unga kwa jivu;

212. Ule mwana kwa swahihi
Kajibu " Nimefurahi
Mentendeya Ilahi
Haya menijaaliya.

Baada ya tukio hilo, mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo hakuweza kurudi kwa mama yake na baada ya muda si mrefu, alipata maradhi ambayo yalisababisha kifo chake;

179. Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t`ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya

223. Siku chache kitimiya
Maradhi yakamngiya
Yasiyomuondokeya
Naye kisa kaifiya.

Baada ya mtoto kumuuwa baba yake, kosa kubwa la kuuwa binaadamu, jamii iliyomzunguka mtoto huyo, haikuridhia; ikawa hiyo ni sababu iliyomfanya kupata kibuhuti na mwisho kufariki. Fumo Liyongo alisalitiwa na mtu wake wa karibu. Kikulacho ki nguoni mwako, mwendani wa mtu ndiye nduwi yake.

4.3.5 Sada

Sada ndiye aliyekuwa akimpelekea Liyongo chakula, wakati alipokuwa kifungoni kwa Mfalme. Binti huyo, alifanikisha mpango wa Liyongo wa kutoroka gerezani. Sada ndiye aliyepewa ujumbe na Liyongo kuambiwa mama yake, amtengezee mkate na ndani atiye tupa;

104. Kamba " Sada nakutuma
Enda kamwambie mama
Afanye mkate mwema
Kati tupa aitiya.

Sada ni mmoja, kati ya wahusika ambao walijitoa muhanga katika kumsaidia Fumo Liyongo. Sada hakusita kumpelekea Fumo Liyongo mkate wenye tupa, ili apate kutoroka.

4.3.6 Askari

Hawa ni walinzi katika gereza la Mfalme. Walinzi hawakuwa waadilifu. Chakula chochote kizuri kilichopelekwa kwa ajili ya Liyongo, walikichukuwa na kukila wao. Kibaya walikitoleya kejeli na matusi. Tabiya yao hiyo, ndiyo iliyowafanya kuudharau mkate aliopelekewa Liyongo, ambao ulikuwa umetiwa tupa ndani yake;

101. Na mamake kwa hakika
Chakula chema kipika
Asikari humpoka
Chakula wakailiya.

Mfalme wa Pate, alitumia chombo hicho cha dola, kuwatia nguvuni na kuwadhibiti wote waliokuwa wanapinga utawala wake.

4.3.7 Wagala

Hawo walikuwa ni raia wa kawaida katika jamii ya Pate. Wahusika hawo waligawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza, ni la wale waliokuwa tayari kumuunga mkono Liyongo kwa hali yoyote, na hawo, baada ya kifo, walihuzunika sana;

226. Mui walisikitika
Hakuna wa kutosheka
Kwa Liyongo kutoweka
Imeanguka pazia

Kundi la pili, ni la wananchi waliomsaliti Liyongo. Hawo ni wale waliokubali utumwa wa Mfalme, ili, wamuue Liyongo. Ubeti wa 86, inatuthibitishia hali hiyo kama ifuatavyo;

86. Wakanenda kwa utungo
Mafumo, zembe, zigongo
Wakamshika Liyongo
Gerezani akatiwa.

4.4 Matumizi ya lugha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), matumizi ya lugha katika Utenzi ni ya kipekee yakilinganishwa na matumizi ya lugha katika bahari nyengine. Kwa mfano, mtunzi wa Utenzi, ana uhuru mkubwa sana katika matumizi ya lugha, uteuzi wake wa msamiati, ubunifu wake, kubuni msamiati wake au maneno unde, kuyaendeleza maneno kwa njia tafauti. Utendi/Utenzi una kawaida ya kutumia maneno ya kale. Pia, mtunzi ana uhuru wa kuipinduwa miundo ya mitongoo. Miundo hiyo, inaweza kusababishwa na nia ya

kupata upatanifu wa kiarudhi au sababu ya kibalagha. Unapogeuzwa muundo wa mtongoo wa kawaida, husisitiza kinachotangulia mwanzoni.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia lugha ya Kswahili, ya Kiamu. Hili linathibitika kutokana na matumizi ya maneno ambayo yametokana na Kiswahili hicho cha Kiamu. Katika sehemu hii, mtafiti alichunguza namna lugha ilivyotumika katika tenzi teuliwa.

4.4.1 Tashibiha

Tamathali hii ya usemi hulinganisha vitu viwili ambavyo havihusiani, kwa kutumia maneno kama vile; kama, mithili, kwa mfano, sawa sawa, mithili. (Njogu na Chimera, 2008). Mbinu hii inapotumika, msomaji au msikilizaji huweza kuchora taswira akilini mwake, jambo ambalo linarahisisha kueleweka kwa kile kinachozungumzwa.

Kuna matumizi ya tashibiha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, kama inavyojitokeza katika vipengele vifuatavyo;

13. Ni mwanamume sahihi
Kama simba una dhihi
Usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya.

Katika ubeti huo, Fumo Liyongo, anamithilishwa na simba, kutokana na ushujaa wake. Katika hadithi na tendi nyingi za Waswahili, mhusika simba, humithilishwa na mhusika anayekubalika katika jamii ya Waswahili, ili kuonesha ushujaa alionao.

Tashibiha nyengine katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, imetumika katika ubeti wa 112;

112. Na ngoma na nyingi kusi
Kusisalie unasi
Ikawa kama harusi
Watu wakiangaliya.

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, kuna matumizi makubwa ya tashibiha. Beti nyengine ambazo zimetumia tashibiaha ni za 47, 55, 111, 157, 177 na 181.

4.4.2 Mubalagha

Matumizi ya mubalagha pia, yamejitokeza katika baadhi ya beti za *Utendi wa Fumo Liyongo*. Hali hiyo, inaibua udadisi wa ukhalisia wa kile kinachozungumziwa katika akili ya msomaji au msikilizaji. Mubalagha unajitokeza katika beti zinazomsifu Fumo Liyongo. Kwa mfano;

12. Mfalume kawambiya
Wagala kiwasifiya
"Huwegemea watu miya
Wasiweze kukimbiya".

Maelezo ya mfano wa hapo juu, yametiwa chumvi. Katika hali ya kawaida, binadamu hana uwezo wa kuwaegemea watu mia, na watu hao wasiweze kujikukusa. Kimsingi, chuku hiyo, imetumika, ili, kumuonesha namna Fumo Liyongo alivyokuwa shujaa katika jamii.

Katika ubeti wa 107, unajengwa picha ya mkate aliwopelekewa Fumo Liyongo gerezani. Mkate huo ulikuwa na uzito wa pishi mbili. Maelezo ya mkate huo yametiwa chumvi. Uswahilini, hakupikwi mkate wenye kiwango cha pishi mbili.

107. Mkate huu sikiya
Pishi mbili hutimiya
Kati tupa akatiya
Liyongo kampekeya.

Vile vile, matumizi ya chuku katika *Utendi wa Fumo Liyongo* yanajitokeza katika beti za; 13, 14, 15, 26, 27, 28, 30, 31, 37, 38, 39, 65, 117 na 183. Beti zote hizo, kwa kiasi kikubwa zimetiwa chuku, ili, kuelezea ushujaa aliyokuwa nao Fumo Liyongo.

4.4.3 Sitiari

Kuna matumizi ya taswira katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Katika ubeti wa 46, mnaelezwa namna mke wa Fumo Liyongo alivyopata ujauzito na akajifungua mwana simba;

46. Mke katukua mimba
Akazaa mwana simba
Mwanamume wa kutamba
Mwane Liyongo sikiya.

Ulinganishi huo, haukutumia aina yoyote ya kiunganishi cha kulinganisha kati ya mtoto aliyezawa na simba. Maelezo hayo yametumika, kuonesha mfanano wa tabiya ya mtoto aliyezawa akilinganishwa na simba. Katika jamii za Waswahili, sitiari hiyo, huwa na maana ya mtoto huyo, alikuwa shujaa na mwenye nguvu, kama za simba.

4.4.4 Kinaya

Njogu na Chimera (1999), kinaya ni tamathali ya usemi, inayohusisha ukinzani katika hali ilivyo. Kinaya ni kauli ambayo ina maana ya kinyume. Kinaya katika Utenzi hujitokeza kwa njia ya majibizano yanayoonesha kinyume cha matarajio au matumaini ya mhusika. Kinaya huwa na pande mbili, upande wa msemaji na upande wa msikilizaji. Msemaji ana maana tafauti na anavyotarajia msikilizaji. Dhima kuu ya kinaya ni kuibua ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia kinaya katika beti za 134, 135, 136, 137, 138 na 139. Kwa mfano:

138. “Baba ukifa yakini
Mimi t`akwenda kwa nyani
Nitakuwa maskini
Wa chakula kuzengeya.

139. “Tanipa kula ni nyani
Na nguo za muilini
Nipate na masikani
Pahala kupumulia.

Mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo, anaeleza, hawezi kutoa siri ya kile kinachoweza kumuua baba yake. Anatoa sababu kwa kusema, yeye ndiye anayemleya, anayempa kula, anayempa makaazi na anayemuhudumia kwa nguo. Wakati anayazungumza hayo, maneno hayo yalikuwa ni kinaya, kwani, ukweli sivyo ulivyokuwa. Nia ya mtoto huyo, ilikuwa kupata siri hizo, ili, kumpelekea Mfalme.

Kinaya kilichojengwa kwa mtoto wa Fumo Liongo, kililenga kueleza namna vijana wengi walivyo na tamaa ya kutaka utajiri wa haraka bila ya kujali utu. Hali kama hiyo, ndiyo iliyomsukuma mtoto wa kambo wa wa Fumo Liyongo kufanya usaliti kwa baba yake, ili apate kile alichoahidiwa na Mfalme.

Aidha, matumizi ya kinaya yanajitokeza katika ubeti wa 55 ambapo kunajitokeza kinaya wakati wa mazungumzo kati ya Wagala na Fumo Liyongo;

55. “Wewe ni kama bwanetu
Tena kasha ni babetu
Uwe ni rafiki yetu
Kula na kunwa pamoya.

Wagala walipokutana na Fumo Liyongo, walivyosema kinyume na yale waliyoyakusudia nyoyoni mwao. Wagala, walimsifu Fumo Liyongo, wakimwambia kuwa, awe Bwana wao, awe baba yao na awe ni rafiki yao. Hata hivyo, maneno yote hayo, yalikuwa yanaelezwa kinyume.

4.4.5 Taswira

Matumizi ya taswira, pia, yamejitokeza katika baadhi ya beti za *Utendi wa Fumo Liyongo*, hali ambayo inaibuwa hisia au vionjo kuhusu jambo hilo katika akili ya msomaji au msikilizaji. Hali hii inamfanya msikilizaji aone, asikie, au apende kile kitu kinachozungumziwa.

Utendi wa Fumo Liyongo, umetumia taswira. Katika beti za 36, 37, 38, na 39 kuna matumizi ya taswira yanayojenga picha ya Fumo Liyongo namna alivyochukuwa vitu wakati alipokwenda Pate;

37. Kisa katiti katuwa
Mkobani akatowa
Zitu alizotukuwa
Nyumba ndima nisikiya.

38. Katowa kinu na mt`i
Na jiwe la kupaza kuti
Na zunguze si katiti
Na mawe ya kupikiya.

Katika mfano huo, msikilizaji anapata picha ya namna Fumo Liyongo alivyokuwa. na nguvu zisizokuwa za kawaida. Nguvu hizo zinaoneshwa kwa kupitia taswira ya vitu alivyovichukua;

Pia, matumizi ya taswira yanajitokeza kwa mfano ubeti wa 202;

202. Kipata siku katiti
Kaanguka ni maiti
Wakatambua umati
Liyongo ameifiya.

4.4.6 Balagha katika *Utendi wa Fumo Liyongo*

Oyoyo (2013), Balagha ni mbinu, ambayo hujitokeza katika fasihi, pale ambapo, mtunzi au mhusika huuliza maswali kwa lengo la kumtanabahisha msomaji au msikilizaji.

Maswali hayo huulizwa bila majibu. Dhima ya maswali ya balagha ni kutoa mawazo au hisiya za ndani za mhusika au kuweka jambo wazi kwa hadhira, na ambalo linahitaji kuangaziwa kwa umakini. Aidha, maswali ya balagha hutumiwa kusisitizia wazo ambalo mtunzi hakudhamiria kulieleza tu au kulitaja bayana.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mbinu hii ya masuali ya balagha;

142. “Kuiyuta kinyumeni
Hela baba hufaani?
Ni kweli nimezodhani
Na yangawa t`akwambiya.

Swali lililoulizwa na Fumo Liyongo, kumuuliza mtoto wake, ni mfano wa swali la kibalagha kwa sababu, Fumo Liyongo alikuwa anamtanabahisha mtoto wake na yale yatakayompata baada ya kufanikisha mpango wake. Hata hivyo, Fumo Liyongo alikuwa hahitaji kupata jibu kutokana na swali hilo. Jibu likapatikana mwishoni, baada ya mtoto, kupokwa uhai wake.

4.4.7 Tabdila

Tabdila ni mbinu ya kuliendeleza neno kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Mbinu hii hutumiwa sana katika Utendi/Utenzi kwa madhumuni ya kuwa na vina au mizani vinavyotakiwa. Msingi wa tabdila ni kubadili muundo.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mbinu ya tabdila. Maneno mingi katika utenzi huo yamebadilishwa, ili kupatikana kwa sauti na mizani sawa. Kwa mfano:

1. Bismillahi nabutadi
   Kwa ina la Muhammadi
   Nandikie auladi

Nyuma **watakaokuya.**

Katika mfano hapo juu, neno **“watakaokuya**” badala ya neno **“watakaokuja”**, katika ubeti wa kwanza, kama inavyoonekana hapo juu, lina sifa ya tabdila. Neno hilo, limebadilishwa, ili kufuata bahari ndogo ya Utenzi huo. Asili ya neno hilo ni “**watakaokuja”** kwa Kiswahili cha Kusini. Kwa huko Kaskazini, *kuya*, badala ya *kuja*, ni matamshi ya kawaida.

4.4.8 Mazida

Mbinu ya mazida ni mbinu ya kurefusha. Neno linaongezewa sauti ama silabi bila ya kubadilishwa maana yake. *Utendi wa Fumo Liyongo*, umetumia mbinu ya mazida. Baadhi ya maneno yamezidishwa, ili kuweka usawa katika sauti;

101. Na mamake kwa hakika
Chakula chema kipika
Asikari humpoka
Chakula **wakailiya.**

Katika msitari wa mwisho, neno **“wakailiya”** badala ya neno **“wakajiliya”,** limekusudiwa, kufuata usawa wa sauti na ndivyo Wa-Amu, wasemavyo.

4.4.9 Iksiri

. *Utendi wa Fumo Liyongo* umetumia mbinu ya ikisari;

97. **“Mekwambia** Bwana wetu
Menituma mimi mtu
Muhula wa siku tatu
Fahamu utauwawa.

Hapo juu, iksiri imetumika katika mshororo wa kwanza, katika neno **“mekwambia”** badala ya **“amekwambia”.** Pia, katika mshororo wa pili, neno “**menituma**` badala ya

neno **“<u>a</u>menituma**”. Katika maneno hayo, silabi “**a**” ya nafsi ya tatu umoja, iliyojitokeza mwanzoni mwa kitenzi, imedondoshwa ili kupatikana kwa mizani sawa.

4.5 Muundo katika Utendi wa Fumo Liyongo

Njogu na chimera (1999), wanasema muundo wa Utendi/Utenzi, hubainishwa kwa kuchambua misitari, beti, mizani na vina. Urefu wa mshororo, hutegemea idadi ya mizani. Urefu wa beti nao hutegemea idadi ya misitari katika kila ubeti. Katia kipengele cha muundo, mtafiti alikusanya data na kuzichambua na kugunduwa yafuatayo;

4.5.1 Mishororo

Mishororo ni misitari katika ubeti wa Utendi/Utenzi. *Utendi wa Fumo Liyongo* una jumla ya beti 232. Kila ubeti umejengeka kwa mishororo mine. Aidha, kila mshororo wa Utenzi huo, una mizani 8;

1 2 3 4 5 6 7 8

201. Ma/ma/kwe/ ki/t a/ a/ ja /bu
Akinena ni ajabu
Mara hini meharibu
Ameiza kusikiya.

1 2 3 4 5 6 7 8
57. Ki/ ko /wa / tu/le/ ma/ ko/ ma
Kukuta hatutokoma
Kula tukiiterema
Kulla mtu siku moya..

4.5.2 Bahari ndogo

Utendi wa Fumo Liyongo, umefuata kanuni ya bahari ndogo ya Utenzi wa Kiswahili, tangu mwanzo mpaka mwisho wa Utendi huo. Umetumia bahari ndogo “**ya**”, ingawa kuna beti chache katika Utendi huwo zimekiuka kanuni hiyo. Kwa mfano;

14. Ghafula kikutokeya
Mkoyo hukutokeya
Tapo ukakuwiliya
Ukutapo na kuli**<u>ya.</u>**

50. Liyongo akatambuwa
Huzengea kuuwawa
Pale Pate kayepuwa
Barani akitembe**ya.**

Aidha, mtafi amegunduwa beti za 27, 30, 78, 86, 91, 170 na 169, ambapo katika beti hizo, bahari ndogo ni **"wa"** ama **"a".** Kwa mfano;

167. Kimkanda maguuni
Pamoya na muilini
Kwa utofuwe ndiani
Maanaye kumto**a**

27. Liyongo kenda muini
Akipata mlangoni
Panda katia kanwani
Kivuzia kapasu**wa**.

Kwa maoni ya mtafiti, kwa vile beti za 27, 30, 78, 86, 91, 170 na 169, ndizo zimekiuka kanuni hiyo ya kale, ya bahari ya Utendi wa Kiswahili, ni dhahiri kwamba, kuna tatizo la unukuzi. Yaelekea mkusanyaji wa Utendi/Utenzi huo, alinukuu kimakosa katika beti hizo.

4.5.4 Mizani

Mizani ni idadi ya silabi katika msitari wa Utendi/Utenzi. Data zimeonesha kwamba, *Utendi wa Fumo Liyongo* umetumia misitari yenye mizani nane kutoka ubeti wa 1-132. Kwa mfano;

1 2 3 4 5 6 7 8

58 Sha/ u/ ri/ li/ ki/ sa/ la/o
Wa/ke/ne/nda/ kwa/ ki/ka/o
M/ko/ma/ wa/u/pa/ta/o
Hu/pa/nda /m/tu /m/mo/ya

97. “Mekwambia Bwana wetu
Menituma mimi mtu
Muhula wa siku tatu
Fahamu utauwawa..

4.5.5 Vina

Vina ni silabi za mwisho katika mshororo wa Utendi/Utenzi. Utendi wa Fumo *Liyongo*, una vina vilivyofanana katika misitari mitatu ya mwanzo kutoka ubeti wa mwanzo hadi ubeti wa mwisho.

14. Ghafula kikutoke**ya**
Mkoyo hukupote**ya**
Tapo likakuwili**ya**
Ukatapa na kuliya.

Vile vile, katika msitari wa mwisho, kuna mfanano wa vina, kutoka ubeti wa mwanzo hadi ubeti wa miwisho, ambapo, kina hicho, ni “*ya*” isipokuwa katika beti za 27, 30, 78, 86, 170, 203, 91 na 169 ambapo katika beti hizo kina cha mwisho ni “*wa*.”

201. Mamakwe kitaajabu
Akinena ni ajabu
Mara hini meharibu
Ameiza kusiki**ya.**

57. Kikowa tule makoma
Kukuta hatutokoma
Kula tukiiterema
Kulla mtu siku mo**ya.**

Mtafiti anaona kwamba, beti hizo hazikukiuka kanuni tangu asili, bali, kuna dalili lilikuwa ni kosa la kiunukuzi.

4.6 Mtindo katika Utendi wa Fumo Liyongo

Njogu na chimera (1999), wanaeleza kuwa, mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwengine. Wanataalimu hao wanaeleza kuwa, unapochunguza mtindo katika Utendi/Utenzi, inapasa kuchunguza matumizi ya maneno yaliyotumika;

iwapo maneno hayo ni maneno magumu, ya kiasili, ya kale, na sababu za kuyatumia maneno hayo. Pia, inahitajika kuchunguzwa, iwapo mtunzi amechanganya lugha. Vile vile, mtindo hutambulikana kwa kuchunguza mishororo ya Utenzi na takiriri zilizojitokeza. Aidha, mtindo hutambulika kwa kuchunguza namna utungo huo ulivyoumbika. Kwa hivyo, mtafiti alikusnya data zinazohusiana na mtindo na kuzifanyia uchambuzi kama ifuatavyo:

4.6.1 Mianzo ya kifomula

Utendi wa Fumo Liyongo umefuata mtindo wa mianzo na miisho ya kifomula. Utenzi huo, umeanza kwa duwa ya kumuaomba Mwenyenzi Mungu;

1. Bismillahi nabutadi
   Kwa ina la Muhammadi
   Nandikie auladi
   Nyuma watakaokuya.

Pia, *Utendi wa Fumo Liyongo* umemalizia kwa duwa ya kumtukuza na kumuomba Mwenyezi Mungu. Hali hii inajidhihirisha katika ubeti wa 229, kama ifuatavyo:

229. Rabi tatusahiliya
   Na uzito wa duniya
   Tena tatujaaliya
   Kuwa njema yetu niya.

4.6.2 Kiswahili cha Asili

Kuhusu lugha iliyotumika, mtafiti amegunduwa kuna matumizi makubwa ya Kiswahili cha Asili hasa lugha ya Kiamu. Kwamujibu wa Kipacha (2003), Kiamu ni miongoni mwa Kiswahili, kinachosemwa katika visiwa vya Lamu. Lugha hii huzungumzwa katika Kisiwa cha Amu (Lamu), ambacho kiliitwa, “Kiwa-ndeo”, yaani kisiwa cha majivuno. Ingawa baadhi ya watafiti kama vile; Bakri (1985), anaeleza kwamba, lugha ya Kiamu na lugha ya Kipate ni lugha moja tu, huku watafiti kama vile, Stigand (1915),

ananukuliwa na Kipacha (ameshatajwa), akieleza kuwa, lugha hizo ni tafauti kabisa. Katika uchunguzi huu, mtafiti ameona kuwa, lugha ya Kipate ni sawa na lahaja ya Kiamu, zina tafauti ndogo ndogo zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa maeneo hayo mawili tafauti. Kama ; da, de, di, do, du, hukazwa sana kwenye Kipate tafauti na ilivyo kwenye Kiamu.

Utendi huo umetumia lugha ya asili, kutokana na uasili wa kisa cha Fumo Liyongo. Aidha, wanajamii, hiyo ndiyo lugha yao, waliyokuwa wakiitumia, na bado inatumika hadi leo katika eneo hilo. Beti za 14 na 50 zinadhihirishia misamiati ya lugha ya Kipate kama ifuatavyo:

14. Ghafula kikutokeya
Mkoyo hukupoteya
Tapo **likakuwiliya**
Ukatapa na kuliya

50. Liyongo akatambuwa
Huzengea kuuwawa
Pale Pate **kayepuwa**
Barani akitembeya.

Beti hizo hapo juu, yaani ubeti wa 14 na 50, kuna matumizi ya maneno ya lugha ya Kiamu. Kwa mfano, katika ubeti wa 14, neno **`mkoya`**, lina maana ya **`mkojo`**, na neno **"ukakuwilia,"** lina maana ya "**kutetemeka**". Aidha, katika ubeti wa 50, neno "**kapepua**" lina maana ya "**akajiepusha**". (Mulokozi, 1999), Baadhi ya beti zilizotumia maneno ya Kiamu, ni beti za ;1, 2, 3, 6, 7, 8, 9, 11, 12, 13, 14, 15, 16, 17, 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25, 27, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 39, 40, 42, 43, 44, 45, 46, 47, 48, 50, 51.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia, kwa kiasi kikubwa, misamiati ya Kiswahili cha Kiamu kama beti 184.

4.6.3 Takiriri

Takiriri ni mbinu ya kukariri neno au maneno fulani. Ingawa Wamitiala (2008), anaeleza kuwa, takiriri ni kukariri neon. Fasili hiyo ni finyu. Mdungi (2001), takiriri ni mbinu ya kurudiya rudiya silabi, neno, misitari au vifungu vya maneno. Pamoja na takiriri kuwa na madhumuni ya kusisitiza jambo kwa kuchezea maneno, pia, huleta uwiano wa sauti za aina moja katika Utenzi.

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo* takiriri imejitokeza kwa kiwango kikubwa. Takiriri zilizochunguzwa na mtafiti ni **takiriri neno** na **takiriri kina.** Aina hizo za takiriri zimejitokeza kama ifuatavyo:

4.6.3.1 Takiriri Neno

Aina hii ya takriri, imejitokeza katika beti kadhaa. Kwa mfano:

5. **Niweleze** kwa utungo
   Hadithi yake Liyono
   Niweleze na mazingo
   Mambo yalomzingia

Matokeo ya takiriri neno imejidhihirisha na kufanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

Neno **`*Wagala*`** limerudiwarudiwa katika beti za 39, 44, 12, 16, 40, 19, 34,na 31. Pia, neno **`*kiivuzia*`** limerudiwarudiwa katika beti za 27 na 28. Vile vile, neno ***Liyongo*** limetumia mbinu hii katika beti za; 5, 6, 10, 11, 18, 20, 21,23, 26, 27, 29, 30, 32, 36, 43, Kwa mfano;

39. Na kipeto cha mtama
    Na ya nazi makoroma
    Wagala wakaatama
    Ajabu ikawangiya.

40. **Wagala** wakabaini
Kumwambia Sulutwani
“Twamtaka kwa thamani
Kijana kutuweleya”.

Takiriri nyengine ya neno ni neno `***Mfalme***` ambalo limefanyiwa takriri katika beti za; 12, 18, 32, 49, 52, 53, 205, 209, 211, 213, na 216. Pia, neno ***Sulutani*** limetumika kwa takiriri na kujitokeza katika beti za; 42, 43, 51, 69, 70, 78, 80, 83, 85, 91, 92, 96, 98, 100, 107, 119, 120, 121, 122, 124, 129, 150, 151,153,158, na 207, kwa mfano;

52.**Mfalume** changaliya
Mwituni mekimbiliya
Wasanya kawazengeya
Na Wadahalo pamoya.

53. **Mfalume** kawambiya
“Liyongo kunipatiya
Kitwa mukanieteya
T`awapa riale miya”.

Matumizi ya takiriri pia yametumika katika neno `***Pate`.*** Neno hilo limejitokeza katika beti za; 71, 76, 145, 149, 205 na 230. Aidha, neno ***“mama”,*** limejitokeza katika beti za; 101, 102, 103, 104, 106, 110, 148, 189, 191, 195, na 196. Neno ***“mui”***, limejitokeza katika beti za; 70, 75, 89, 226, 231 na 232. Kwa mfano:

71. Mwambieni, `Tusafiri
Hata Pate tukajiri
Hapana tena khatari
Habari tumesikiya.
76. Liyongo akasikiya
Naye akaazimiya
Wakenenda kwa umoya
Hata Pate wakangiya.

Kwa jumla, mtafiti amegunduwa kuwa, kuna maneno mengi yametumia mbinu ya takiriri. Maneno hayo ni pamoja na; katiti, kusi, mkoma, ngoma, simba, miya miya, gungu, sharuti, panda, khatari, siri, chakula asikari, mkate, mwao, gerezani, gheri, wishwa, Sada, Mashaka , bawabu, shaka, mimi, sindano, kapanda, babake, baba, kijana, idhini, harusi, uta, shauri, mamakwe, ada, Mngu, tena na tupa.

Mtafiti amegunduwa kwamba, matumizi ya takiriri neno, ni mbinu inayotumiwa na tendi za Kiswahili katika mtindo wa kazi hizo.

4.6.3.2 Takiriri Kina

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kuna matumizi ya *takiriri kina*. Hii ni aina ya takiriri silabi. Hivyo, *takiriri silabi*, mtafiti alizozishughulikia ni *takiriri vina* ambazo hujitokeza katika kila mwisho wa mshororo. Takiriri za kina zimelingana katika misitari mitatu ya mwanzo katika kila ubeti. Takiriri za aina hiyo, hukamilisha kanuni na ujumi wa Utendi wa Kiswahili. Silabi hizo zinaifanya misitari iimbike kwa sauti ya aina moja, na kufanya mvuto miongoni mwa wasikilizaji. Kwa mfano;

231. Na kwa Mwana ni Rasi**ni**
Ya Shaka iyuwe**ni**
Ni mui hapo zama**ni**
Ni mkuu hukwambiya

232. Mui waloamiri**ka**
Nyumba za mawe hakika
Mayiwe waliyawe**ka**
Na misikiti pamoya

Pia, kuna matumizi ya silabi "**ko**" , katika beti za; 160, na 210, silabi "**di**", imetumika katika beti za; 1, 22 na 222. Aidha, takiriri ya silabi "**ri**", imejitokeza katika beti za; 3, 64, 71, 74, 88, 90, 103, 114, 175, 217 na 219. Aidha, takiriri ya silabi "**ya**", imejitokeza katika beti za; 12, 14, 15, 19, 32, 34, 42, 49, 52,53, 60, 76, 82, 102, 107, 110, 118, 119, 122, 133, 136, 144, 145, 148, 158, 172, 173, 166, 189, 190, 194, 195, 198, 199, 203, 205, 211, 218, 223, 229, 230 na 232. Kwa mfano:

1. Bismillahi nabutadi
Kwa ina la Muhammadi
Nandikie auladi
Nyuma watakaoku**ya.**

12. Mfalume kawambiya
Wagala kiwasifiya
"Huwegema watu miya

Wasiweze kukimbi**ya.**

Vile vile, takiriri silabi "**ni**", imejitokeza katika beti za; 9, 11, 27, 40, 67, 29, 54, 65, 70,72,78, 80, 83, 87, 96, 98, 100, 125, 126, 109, 120, 121, 134, 135, 138, 139, 142, 150, 151, 162, 165, 167, 169, 179, 186, 191, 196, 200, 204, 206, 208, 213, 220 na 231, kwa mfano:

9. Wagala hao yuwani
Ni wakuu wa mwituni
Kabila la sulutwani
Mashujaa wote piya.

Pia, silabi "**ka**", imefanyiwa takiriri, katika beti za; 16, 18, 20, 25, 28, 43, 84, 85, 101, 105, 111, 113, 130, 131, 132, 141, 149, 153, 156, 168, 176, 180, 188, 197, 207, 124, 226 na 227, kwa mfano;

16. Wagala wakipulika
Kwa dhihaka wakateka
Wakanena "twamtaka
Na sisi kumwangaliya"

Silabi "**wa**", nayo imefanyiwa takiriri katika beti za; 24, 37, 48, 50, 94, 127, 140, 177, 192, 209 na 216. Pia, silabi "**ma**" imejitokeza katika beti za; 39, 57, 61, 66, 104, 182, 184 na 193. Vile vile, silabi "**na**", imefanyiwa takiriri katika beti za; 10, 33, 56, 63, 68, 77, 89, 91, 95, 108, 124, 154 na 221. Takiriri nyengine ni silabi "li" katika beti za 6, 23, 26, 30, 99 na 146. Aidha, silabi "**bu**", imefanyiwa takiri katika beti za ; 21, 69, 123, 137 na 201. Kwa mfano;

24. Kaifunga kwa sitawa

Silaha za kuteuwa
Panda tatu katukuwa
Kaziwangaa pamoya

39. Na kipeto cha mtama
Na ya nazi makoroma
Wagala wakaatama

Ajabu ikawangiya.

Matumizi mengine ya takiriri, yanajitokeza kupitia silabi "**ti**".ambayo, imerudiwa rudiwa katika beti za; 17, 36, 38, 155 na 202. Silabi "**ke**", imetumika katika beti za; 41, 81, 147, 170, 181 na 183. Silabi "**o**" imefanyiwa takiriri katika beti za; 58, 59, 73, 79 na 185, na silabi "**tu**", imefanyiwa takiriri katika beti za; 31, 55, 97 na 225. Kwa mfano;

17. Na yeye alikiketi

Kwa nduze wasi katiti
I huko yake baiti
Kwa Waungwana Mashaa.

41. "Twaitaka mbeu yake
Nasi kwetu tuipeke
Kwa furaha tumuweke
Apate kutuzaliya.

Takiriri nyengine zilizojitokeza ni silabi "**si**", katika beti za; 2, 112, 116, 128 na 157, silabi "**mu**", ambayo imejitokeza katika beti za; 129, 174, 178 na 228, silabi "**za**", katika beti za; 45, 75, 117 na 159, Kwa mfano:

112. Na ngoma na nyingi kusi
Kusisalie unasi
Ikawa kama harusi
Watu wakiangaliya.

129. Sulutwani muadhamu
Kijana kamkirimu
Kwa zakula zilo tamu
Kampa na nguo mpiya.

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, kuna silabi kama vile**; la, fu, ba, ye, po, ko, mba, ndo, i, ngu, ta, ngo me, sha, nda** na **hi**, zimefanyiwa takiriri.

Matumizi ya takiriri katika tenzi za kiswahili hayaepukiki. Takiriri, ndizo zinazoufanya Utendi/Utenzi wa Kiswahili uimbike kwa sauti moja, na iwapo kanuni hiyo itakiukwa, huo utakuwa si Utendi/Utenzi wa Waswahili, utakuwa ni utungo mwengine wa kisanii.

4.7 Upekee wa Utendi wa Fumo Liyongo

Data za utafiti wetu zimeonesha kuwa *Utendi wa Fumo Liyongo* una upeeke wake. Sifa za hizo kipekee za Utendi huo ni kama ifuatavyo:

4.7.1 Shujaa wa Mapisi ya Waswahili

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mhusika shujaa wa mapisi ya Uswahilini, aliyewahi kuwapo katika upwa wa Afrika Mashariki. Wazo hilo linaelezwa pia na Mulokozi (1999) anayeeleza kuwa Fumo Liyongo ni shujaa wa kihistoria aliyewahi kuwapo katika maeneo ya Siu. Katika ubeti wa 230, kunaelezwa mapisi ya Fumo Liyongo kwa ufupi kama ifuatavyo:

230. Ya Liyongo hukwambiya
Siu alikozaliwa
Pate akitembeleya
Kwa Mwana akafiliya.

Matumizi ya shujaa Fumo Liyongo, kama ilivyokwishaelezwa awali na mtafiti, yanaufanya Utendi huo kuwa na sifa ya kipekee, kuwa ni marejeleo ya mapisi ya Waswahili katika eneo la Afrika Mashariki.

4.7.2 Mgogoro wa Utawala katika Eneo la Waswahili

Utendi wa Fumo Liyongo una matumizi ya mgogoro uliyokuwapo katika eneo la Afrika Mashariki. Kwa mfano, inaelezwa kuwa utawala aliopambana nao Fumo Liyongo ni utawala wa Mfalme Fumo Omar (Daudi Mringwari), uliowahi kuwapo katika karne ya 13 katika eneo hilo la Pate. Mgogoro huo ulizuka kutokana na Mfalme kuhofia kunyang`anywa ufalme na Fumo Liyongo. Kwa mfano:

51. Na Sulutwani niseme
Alikucha mwanamume
Tampoka ufalume
Dhana alimdhaniya.

53. Mfalume kawambiya
“Liyongo kinipatiya
Kitwa mukanieteya
T`awapa riali miya”.

4.7.3 Usaliti wa Mtoto kwa Baba yake wa Kambo

Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, kuna tukio la mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo kumsaliti baba yake. Tenzi nyingi za Kiswahili zinawachora wahusika wake wakisalitiwa na maadui wa nnje ya familia zao. Hao, ndiwo huwa na dhima ya kupambana na shujaa. Katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo alimsaliti baba yake;

179. Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t`ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya

4.7.4 Matumizi ya Mhusika mwenye Nguvu na Uwezo wa Kimaajabu

Utendi wa Fumo Liyongo umemtumia mhusika aliye na nguvu na uwezo wa kimaajabu. Fumo Liyongo alikuwa hawezi kudhurika isipokuwa kwa sindano ya shaba ya kuchomwa katika kitovu;

143. Nisikiya wangu baba
Liniuwalo ni haba
Ni msumari wa shaba
Kitovuni nikitiya.

4.8 Hitimisho

Sura hii imeowacha data zilizo kusanywa kupitia kazi teule. Data zimepangwa kutengemea madhuri mahususi ya utafiti. Uchambuzi wa data ulipangwa kutengemea mpagilio wa maswali ya utafiti huu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaelezea khitimisho ya utafiti. Sehemu ya pili inaelezea mapendekezo ya utafiti.

5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulilenga kutafiti, kukusanya na kuchambua data, kuhaki na kufafanua sifa za kifani za Utendi wa Kiswahili. Utafiti ulizingatia vipengele vya fani, yaani muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha, kwa kukusanya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utafiti ulikuwa wa Maktabani. Data zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ujumi wa Kiafrika na Nadharia ya Umuundo. Utafiti huu una umuhimu wa kuelezea sifa za Utendi/Utenzi wa Kiswahili. Pia, utafiti umeweka wazi dhana ya Utendi na dhana ya Utenzi kuwa ni sawa, miongoni mwa Waswahili na zina sifa mahususi. Matokeo ya utafiti huu ni kama yafuatavyo:

5.1.1 Madhumuni Mahsusi ya Kwanza

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza sifa za Utenzi wa Fumo Liyonga. Madhumuni hayo yaliongozwa na swali lisemalo; Utenzi wa Fumo Liyongo una sifa zipi?”

Utafiti wetu umebaini kuwa dhana ya Utendi na Utenzi ni dhana moja miongoni mwa Waswahili. Tafauti kubwa ni ile ya kimatamshi tu. Wapo wanaotamka Utendi (wengi wao wako Kaskazini), na wapo wengine hutamka Utenzi (hasa Kusini mwa Waswahili).

Katika ufafanuzi wao, Njogu na Chimerah (1999) wametumia dhana ya Utenzi huku neno Utendi wakiliingiza katika mabano. Hii ina maana kuwa hata Njogu na Chimera wanakubali kuwa maneno hayo ni visawe vyenye kubeba dhana moja miongoni mwa Waswahili. Kwa hivyo, katika utafiti huu dhana ya tendi imeleezwa sawa sawa na dhana ya Utenzi.

Katika utafiti huu imegundulika kuwa sifa za tendi ni kwamba huweza kuwa na mhusika aliye shujaa au asiye shujaa. Kwa mfano, katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, Fumo Liyongo ndiye mhusika shujaa anayepambana na Mfalme. Zipo tendi za Kiswahili ambazo hazina mhusika shujaa, huweza kuwa na mhusika anayepokea wasia, mawaidha na maaso fulani ya kimaadili, ya dini na hata ya kiuchumi.

Pia, mtafiti amegundua kwamba urefu wa Utenzi/Utendi wa Kiswahili hutegemea kisa. Utenzi huweza kuwa mrefu sana iwapo kisa kinachosimuliwa kina mawanda mapana. Wazo hilo limepingana na mawazo yasiyokubalika ya wale wote wanaoona kuwa utendi lazima uwe mrefu. *Utendi wa Fumo Liyongo* una jumla ya beti 232. Ni kawaida ya kuzoweleka tenzi kuwa ndefu kuliko shairi, lakini Utendi una sifa za kipekee mbali ya hiyo ya urefu au wingi wa beti.

Vielvile, Utenzi wa Kiswahili una sifa ya muundo na mtindo wa bahari ya Utendi. Bahari ya Utendi/Utenzi wa Kiswahili huwa na kina cha bahari ndogo kinachojitokeza mwishoni mwa msitari wa nne katika kila ubeti. Silabi hiyo huwa haibadiliki kutoka mwanzo hadi mwisho wa Utenzi. Aidha, kila misitari mitatu ya mwanzo, huwa na kina cha mwisho kinachofanana katika kila ubeti. Iwapo itatokea utungo uliokiuka kanuni hiyo, huo utaitwa guni ambao utakuwa si Utendi wa kawaida wa Kiswahili.

Aidha, Utendi wa Kiswahili una sifa ya mapisi. Mapisi hayo, huwa ni ya kweli. Ingawa huwa yanaelezwa kwa mbinu ya kisanii. Pia, mapisi hayo huweza kuihusu jamii ya Waswahili au nje ya jamii ya Waswahili. Kwa mfano, *Utendi wa Fumo Liyongo* unaelezea mapisi ya miji ya pwani ya Afrika Mashariki na migongano ya kiutawala iliyowahi kutokea hapo kabla.

Utenzi wa Kiswahili pia una sifa ya uunganifu wa matukio kutoka mwanzo hadi mwisho. Utenzi wa Kiswahili huungana kutoka mwanzo mpaka mwisho huku tukio moja likisababisha kutokea tukio jengine.

Utendi/Utenzi wa Kiswahili huwa na maudhui ya dini ya Kiislamu. Waumini huonywa kutokana na mifumo isiyokubalika mbele ya Mwenyenzi Mungu Mmoja. Mwenyezi Mungu ambaye husifika kwa sifa ya umoja (kupwekeka kwake), Mwenye uwezo wa kila kitu ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa na hahusiki na chochote.

Tendi za Kiswahili zina mianzo na miisho ya kifomula. Tenzi za Kiswahili huanza kwa duwa na kumalizika kwa duwa ya kumuomba Mwenyezi Mungu (S.W). Anayeombwa ni Mwenyezi Mungu Mmoja aliyeumba ulimwengu na vilivyomo ndani yake. Mola anasifiwa kwa sifa ya kuwa ni Umoja, ndiye Mwenye kutegemewa na vyote, Mola ambaye hakuzaa, hakuzaliwa wala hakuna chochote kilichofanana na yeye. Aidha, Mtume Muhammad (S.A.W), ni Mtume na Mjumbe wa Mwenyenzi Mungi. Katika utafiti huu, *Utendi wa Fumo Liyongo* umethibitisha sifa hizo mahususi.

5.1.2 Madhumuni Mahsusi ya Pili

Madhumuni ya pili yalihusu kufafanua vipengele vya fani vinavyojitokeza katika *Utendi wa Fumo Liyongo*. Haya yaliongozwa na swali la utafiti lisemalo: `Je ni

vipengele vipi vya *fani vilivyotumika katika Utendi wa Fumo Liyongo?*` Vipengele vya fani vilivyofanyiwa uchunguzi ni muundo, wahusika, lugha, mandhari na mtindo. Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa data zetu, mtafiti aligunduwa yafuatayo kuhusiana na fani ya utendi huu.

Kwanza, mtafiti amegunduwa kuwa Utenzi huo umetumia lugha ya Kiswahili cha asili cha Kiamu. Kiswahili hicho kipo hadi leo hii katika maeneo ya Lamu, ambako ndiko *Utendi wa Fumo Liyongo* ulikochota mandhari yake. Pia, katika *Utendi wa Fumo Liyongo* kuna matumizi ya vipengele vya lugha kama vile, tashibiha, sitiari, kejeli, mubalagha, balagha, tabdila, iksiri, taswira na mazida. Vipengele hivyo, vimetumika kwa ufundi wa hali ya juu kuhakikisha kwamba Utenzi huo unakuwa na mvuto kwa wasomaji na wasikilizaji wake.

Kuhusu mandhari, mtafiti amegunduwa kuwa *Utendi wa Fumo Liyongo* umetumia mandhari ya maeneo ya Upwa wa Afrika Mashariki. Kwa mfano, mandhari yaliyotumika ni ya kisiwa cha Pate. Pia, kuna matumizi ya mandhari ya gerezani, nyikani na katika nyumba ya Mfalme.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia mitindo kama vile uchaguzi wa maneno ya Kiswahili cha asili cha Kiamu, mtindo wa mianzo na miisho ya kifomula, na mtindo wa kuanza na kumalizia kwa duwa za kumuomba Mola. Kuna matumizi ya takiriri, hasa, takiriri neno na takiriri vina. Lengo la matumizi ya takiriri vina na neno ni kuleta sauti ya aina moja na kuufanya Utendi huo uimbike kwa sauti inayofanana. Kila msitari una mizani nane (8) na misitari mitatu ya mwanzo ina kina cha aina moja, Aidha, kuna kina cha ``ya`` kinachofanyiwa takiriri mwishoni mwa kila msitari wa mwisho wa kila ubeti.

Utendi wa Fumo Liyongo umetumia muundo wa bahari ya Utenzi. Utenzi huo umejengeka kwa misitari mine mine katika kila ubeti, kama zilivyo tenzi nyengine za Kiswahili. Misitari hiyo imeundwa kwa kipande kimoja kimoja tu. Pia, kila msitari una mizani nane (8). Jumla ya beti za Utenzi huo ni 232 ambazo zimekamilisha utungo huo.

Kuhusu wahusika, *Utendi wa Fumo Liyongo* umetumia mhusika shujaa, mhusika hasidi na wahusika wadogo. Mhusika shujaa ni Fumo Liyongo. Mhusika huyo anapambana na Mfalme kutokana na uongozi mbaya wa huyo Mfalme. Mhusika, Fumo Liyongo anasaidiwa na watu wake wa karibu katika mapambano na Mfalme. Fumo Liyongo anasaidiwa na Mama yake na Sada, pia jamii inayomuhurumia. Mhusika hasidi ni Mfalme. Mhusika huyo, anafanya kila njama ili kuhakikisha Fumo Liyongo anauwawa. Mhusika huyo anasaidiwa na Wagala na mtoto wa kambo wa Fumo Liyongo. Mwisho, anafanikiwa kumuua Fumo Liyongo kwa kumtumia mtoto wa Fumo Liyongo aliyemchoma sindano ya shaba kitovuni akiwa usingizini.

5.1.3 Madhumuni Mahususi ya Tatu

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa kuelezea sifa za kipekee za *Utendi wa Fumo Liyongo*. Madhumuni hayo yaliongozwa na swali la utafiti lisemalo ` *Utendi wa Fumo Liyongo una sifa zipi za kipekee?*` Baada ya mtafiti kuzifanyia uchunguzi na kuzichambua data alizozikusanya, *Utendi wa Fumo Liyongo* ulionekana kuwa na upekee. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Utenzi huo unatumia mhusika shujaa wa kimapisi, anayeaminika kuwako katika Upwa wa Afrika Mashariki, hasa katika eneo la Pate. Kwa mfano, Mulokozi (1999) anaeleza kuwa kitabu cha tarehe ya Pate kinamtaja mtawala wa eneo la Ozi, aitwaye Fumo Liyongo, aliyeishi wakati wa utawala wa Fumo Omar. Utendi huo pia umetumia mhusika asiyedhurika isipokuwa kwa msumari wa shaba katika kudungwa kitovuni mwake. Matumizi ya mhusika asiyedhurika, isipokuwa

kudungwa msumari wa shaba kitovuni mwake, ni mtindo wa kipekee miongoni mwa tenzi za Waswahili.

Pia, *Utendi wa Fumo Liyongo* una upekee kutokana na kuwa na mhusika anayemuua baba yake wa kambo kwa njama za kuhadaiwa na Mfalme. Aidha, hadi sasa mtafiti hakuona Utenzi mwengine uliotumia mbinu kama hiyo.

5.2 Hitimishi

Utafiti huu ulilenga kutafiti, kuchunguza na kuchambua data zinazohusiana na Sifa za Kifani za Utendi wa Kiswahili: Mfano *Utendi wa Fumo Liyongo*. Sifa za kifani za Utendi wa Kiswahili zilionekana hazijafanyiwa utafiti wa kina. Hali hii ilipelekea mtafiti kuona ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kupunguza pengo hilo la kitaaluma.

Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, Utendi wa Kiswahili una sifa ya muundo wa ushairi unaofuata bahari ya Utendi, una mianzo na miisho ya kifomula (kuanza na kuishia kwa duwa), hauna urefu mahsusi au idadi maalumu ya beti na si lazima uwe na mhusika shujaa. Sifa nyengine ni kuwa na uunganifu, maudhui ya dini ya Kiisilamu na mapisi ya kweli.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Tunatoa mapendekezo kwa asasi na wadau mbalimbali.

5.3.1 Kwa Watunga Mitalaa

Waanze kutenganisha dhana ya Utendi/Utenzi na dhana ya epiki kwani dhana hizo ni tafauti.

5.3.2 Walimu

Walimu kwa jumla yao wazingatie na waangalie kwa kina tafauti ziliopo kati ya Utendi na epiki ili wasiendelee kuzifundisha dhana hizo kimakosa.

5.3.3 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar iiombe Serika ya Mapinduzi Zanzibar kujenga maktaba zitakazosaidia upatikanaji wa marejeleo kwa tafiti za viwango vya Uzamili na Uzamivu.

MAREJELEO

Applebee, N. A. na wenzake. (2000). *The Language of Literature: British Literature*. United State of America. McDougal Littelll Inc

Biebuyck, D. P. (1972). *The Epic as a Genre n Congo Oral Literatur.* In Dorson

Chaligha, E. N.(2013). "*Vigenzo vya Ruth Finnegan katika Utendi wa Lianja."* Dar es Salam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 32, 82-91

Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurement:* Educational Psychology.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: Clarendon

Foibe, N. (2013). *Taswira ya Kifo cha shujaa katika Utendi: Shujaa Liyongo na* Imani za Jadi na Usasa. Nordrik Journal of African Studies 16 (3) 298-319.

Katagwa, F. L. (2013). *Sifa za Kiuhalisia Ajabu na Umuhimu wake Katika Utenzi wa Mwana Kupona.* Tasnifu ya M.A- Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi

Kijana, P. M. (1987). *Wimbo wa Kanda Mbili.* Dar es Salam: Benedictine Publication Ndanda

King`ei, K. (2001). *Historical and Folkloric Elements in Fumo Liyongo`s Epic.Imepakuliwa kutoka chomboziblogspot.com tarehe 23/5/2014 saa 3.51*

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mayoka, J. M. M. (1977). *Vina na Mizani ni Uti wa Utendi/Utenzi wa Kiswahili*. Katika Mulika Na. 9: 4-11

Mbele, J. (1986). *The Liyongo Fumo Epic and tha Scholars.* Kiswahili 53/1and 2: 128-145

Mbogo, E. (2009). *Fumo Liongo. Dar es Salam:* Dar es Salam Unversity Press

Mdungi, A. (2000). "*Dhana ya Utenzi wa Mapokeo".* Zanzibar: Ministry of Education Katika Jarida la Elimu Zanzibar.Toleo na. 1: 30-37

Muhammad, A. A. (2010). *Tamko Lenye Faida katika Dalili za Kumpwekesha Allah (S.W).* Yemen. Alwadey.

Mnyagatwa, T. K. S. Y. S. (2009). Tungizi za Mnyagatwa. Dar es Salam: Akademiya

Mukuthuria, M. (2007). *Upekee wa Utenzi wa Sifa za Nguvumali: Utenzi wa Mpito, Mseto.* (Tasnifuya M.A Kiswahili, haijachapwa) Nairobi. Chuo Kikuu cha Nairobi .

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

——————— (1999) *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salam: TUKI.

Ndumbaro, E (2013). *Jaala ya Shujaa. Imepakuliwa kutoka* chomboz.blogspot. com/p/fasihi-4html *leo* 18-9-2012, saa 8.10.

——————— (2013). *Uhakiki wa Fumo Liyongo kama Utendi wa Afrika* . Imepakuliwa kutoka chomboz.blogspot. com/p/fasihi-4html tarehe 16-9-2014, saa 7.30.

——————— (2013). *Fasihi Simulizi ya Kiafrika..* Imepakuliwa kutoka chomboz.blogspot. com/p/fasihi-4html tarehe 17-8- 2014, saa 8.00

Ndumbu, N. (2013). *Matumizi ya Takiriri na Sitiari katika Utenzi wa Rasi-lGhuli.* Tasnifu ya M.A Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999*).Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Othman, S.Y. na Yahya, A.S. (2004). *Howani Mwana Howani: Tenzi za Zainab Himid.* Dar es Slam : Press Publishers.

Ouma, O. K. (2013). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Issa (A.S).* Tasnifu ya M.A Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Robert, S. (1966). *Pambo la Lugha (chapa ya tatu).* Nairobi: Oxford University Press

_____ (2013). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini (toleo la nne).* Dar es Salam: Mkuki na Nyota.

Rubanza, Y. I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo.* Dar es Salam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salam: Al-Amin Education and Research Academy.

_____(2007). *Utendi wa Mambo Mambo*. Dar es Salam: Al-Amin Education and Research Academy.

_____ (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Dar es Salam: Al-Amin Education and Research Academy.

_____ (2015). *Sengo na Fasihi za Kinchi : Na 2.* Dar es Salaam. AERA Kiswahili Research Product.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Utenzi Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salam: Dar es Salam University.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salam: Taasisi ya Ukuzaji Mitaala.

TAKILUKI.(1981). *Misingi ya Nadharia ya Kiswaili.* Sweden: Berlings, Arlovs Tanzania.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi : Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Kenya Lithotho Ltd.

_____ (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publisher

NYONGEZA

Kiambatanishi Na. 1: Beti zenye kutumia maneno ya Kiswahili cha Asili cha Kiamu katika Utendi wa Fumo Liyongo

52 . Mfalume **changaliya**
Mwituni mekimbiliya
Wasanye **kawazengeya**
Na Wadahalo pamoya
56. Siku moya wakanena
Na tuleni waungwana
Kikowa ni tamu sana
Karamu **sotindikiya**
59. Na wao maana yao
Siku yeye apandao
Wamfume **wu`te** hao
Zembe kwa wao umoya.
65. Akawambia "Ngojani"
Akatowa mkobani
Chembe katia **ngweni**
Makoma kiwanguliya.
66. Achangusha **ngaa** ndima
Ni **mangi** mno makoma
Kwa **wu`te** wakaatama
Ajabu zikawangiya.
67. Wakanena kwa moyoni
"Amuwezao ni **nyani**
Huyuno hawezekani
Ni kutaka kwangamiya"
69. Sulutwani kabaini
"Hela kamzoezeni
Mumrejeze **muini**
Nimeomba name haya
79. Liyongo nikwambiao
Shaha wa **gungu** na **mwao**
Tena ni mkuu wao
Huwashinda **wu`te** piya.